**MWEKEZAJI** wa kigeni adaiwa kumpiga ngumi mzawa, waziri afunga mgodi
UKURASA 9

**WAVUVI** wanaotumia mabomu wajisalimisha kukwepa kushtakiwa
UKURASA 15



**RUTO** atangaza kubana matumizi, aanza uchunguzi
UKURASA 17


# Nipashe

Jumamosi Julai 6, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581729

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**UNITED YAMPA TEN HAG MKATABA MIAKA MIWILI**
UKURASA 22

# Samia: Kuna kitu nyuma ya mgomo wa Kariakoo

**ATAJA** sababu kumwondoa Kidata TRA, ahimiza ulipaji kodi serikali iache kukopa... *Endelea ukurasa 3*



Rais Samia Suluhu Hassan akimwapisha Yusuph Mwenda kuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ikulu ndogo ya Tunguu, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Utafiti wabaini 86 wametekwa nchini miaka 4, wahusika wake hawajakamatwa
UKURASA 4

**SAKATA LA SUKARI**

## Bodi yavunja ukimya, yajibu hoja zilizoibuliwa na wadau
UKURASA 2

**MICHEZO** **BALEKE ASAJILIWA YANGA** UK 24

**MAONI, KATUNI UK.6**

SAKATA LA SUKARI

# Bodi yavunja ukimya, yajibu hoja zilizoibuliwa na wadau

**Na Romana Mallya**

BAADA ya kuibuliwa hoja mbalimbali kuhusu uagizaji sukari nchini, Bodi ya Sukari Tanzania (SBT) imeibuka kutoa ufafanuzi kuhusu hoja hizo.

Bodi hiyo imesema kuwa serikali haiwezi kuua sekta ya sukari nchini kwa kuwa na yenyewe imewekeza humo na ndio maana viwanda vilivyopo vinaendelea kupanua uwekezaji wake, huku yenyewe ikijenga miundombinu ya barabara, umeme na madaraja.

Pia imesema haikuchelewa kutoa vibali kwa wazalishaji, bali wao ndio walichelewa kuvichukua baada ya kuwa imevitoa kwa ajili yao.

Mkurugenzi Mkuu wa SBT, Prof. Kenneth Bengesi aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akitoa ufafanuzi kuhusu hoja mbalimbali zilizotolewa na wadau.

Ufafanuzi wake ulilenga ubinafsishaji 1998-2001 hadi mwaka 2015, mabadiliko ya Kanuni za Sheria ya Sukari (Bulk Procurement) 2015, mabadiliko ya Sheria ya Sukari, 2020 na hali ya uzalishaji na uingizaji sukari kuziba pengo msimu wa mwaka 2022/23.

Alisema kuwa Julai Mosi mwaka huu, jijini Dar es Salaam, wakati wa mkutano wa Chama cha Wazalishaji Sukari Tanzania (TSPA), kulijitokeza hoja ambazo wameona zijibiwe ili kuweka kumbukumbu vizuri na kuepusha upotoshaji kwa umma.

Hoja hizo ni pamoja na madai ya wazalishaji kucheleweshewa vibali vya kuagiza sukari katika msimu wa mwaka 2022/23, Prof. Bengesi akikanusha madai hayo kwa maelezo kwamba wao wazalishaji sukari ndiyo walichelewa kuchukua vibali vyao toka bodi hiyo.

"Ifahamike kuwa Bodi ya Sukari iliwaandikia wazalishaji kuja kuchukua vibali vya kuingiza sukari tangu Machi 20, 2023. Kampuni ya kwanza (Kilombero) ilichukua kibali Machi 30, 2023 (siku 10 mbele) na kampuni mbili za Kagera na Mtibwa zilichukua Aprili 14, 2023.

"Kampuni ya TPC ilichukua kibali chake Mei 3, 2023 na Kampuni ya Bagamoyo haikuchua kabisa kibali chake.

"Pamoja na kampuni hizo nne kuchukua vibali vyao, ni kiwanda kimoja tu cha Kilombero ndicho kilichoagiza sukari kwa msimu huo kiasi cha tani 2,380 na viwanda vilivyobaki havikuingiza sukari nchini," alisema.

Prof. Bengesi alisema ifahamike kuwa kabla ya marekebisho ya Sheria ya Sukari, Sura ya 251, kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024, kushindwa kwa wazalishaji kuingiza sukari katika msimu wa 2022/23 kuliwapotozea sifa kupewa tena kibali kuingiza sukari nchini msimu wa 2023/2024 kwa mujibu kifungu cha 14(3)(b)(v).

Alisema kuwa kutoingiza kiasi chote cha sukari kilichoidhinishwa kulisababisha nchi kutokuwa na sukari ya ziada katika mzunguko wa soko, hivyo bei ya bidhaa hiyo ikapanda hata kufikia Sh. 4,000 kwa kilo mwezi Juni 2023 na kuchangia kuathirika kwa utengamano wa soko katika msimu wa uzalishaji kwa mwaka 2023/24.

Alisema kuwa kwa msimu wa mwaka 2023/24, kumekuwa na madai kuwa mwaka huu vibali vya sukari vilichelewa kutolewa kwa kampuni za wazalishaji na kampuni za vocha zilipewa kabla yao.

"Taarifa hii si ya kweli kwa kuwa utoaji vibali ulianza na kampuni za wazalishaji Januari 4, 2024 (Kilombero), Januari 5, 2024 (Kagera, Mtibwa na TPC) na Bagamoyo Februari 2, 2024.

"Hizi kampuni za vocha walipewa Januari 30, 2024 baada ya kuona mwenendo wa uingizaji wa kampuni za wazalishaji haueleweki," alifafanua.

Pia alikanusha maelezo yaliyotolewa na Balozi Ammi Mpungwe (Mwenyekiti wa Bodi ya Kilombelo) kuwa kampuni yake ilileta meli yenye tani 4,500 kabla ya kupewa kibali, akiwa na maelezo kuwa wataalamu wake hawakumpa taarifa sahihi.

"Kama kampuni ya Kilombero 'ili-divert' meli yenye tani 4,500, kwanini sukari ya Kilombero iliyoingia ya kwanza ilikuwa tani 265 na kwanini mwezi Januari na Februari kiasi kilichoingia kilikuwa chini ya hizo tani 4,500?" alihoji.

Alisema kampuni zote ambazo zilipewa vibali zilikuwa na leseni halali za biashara ya chakula na hivyo hoja ya jina la kampuni haina msingi na imelenga kuichafua serikali.

"Tuliangalia pia uwezo wa kampuni kuleta sukari katika kipindi ambacho kilikuwa kigumu sana kwetu. Cha ajabu ni kuwa kampuni hizo ambazo zimebezwa na zinaitwa kuwa ni za vocha, ndizo ziliingiza sukari na kutuvusha katika kipindi hiki kigumu na sasa sukari inauzwa Sh. 2,800 kwa kilo kutoka kuuzwa kwa wastani wa Sh. 6,500 kwa kilo.



Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Sukari nchini (SBT), Prof. Kenneth Bengesi akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Kiongozi huyo wa bodi pia alionesha mwenendo wa uingizaji sukari nchini mwaka 2022/23, akieleza kuwa kwa mwezai Februari wazalishaji waliagiza tani 6,070 na wafanyabiashara tani 25,750; Machi wazalishaji waliagiza tani 17,119 na wafanyabiashara 59,073.

Kwa mwezi Aprili, alisema wazalishaji waliagiza tani 15,386 na wafanyabiashara tani 29,235; Mei wazalishaji tani 2,405 na wafanyabiashara tani 29,235 na Juni wazalishaji waliagiza tani 6,183 na wafanyabiashara tani 540.

Alibainisha kuwa mabadiliko ya sheria ya mwaka 2020 yamewezesha uzalishaji sukari nchini kuongezeka na kuchangia zaidi ya asilimia 93 ya mahitaji yenye ubora unaohakikiwa na kuthibitishwa kwa matumizi salama ya majumbani kulingana na mahitaji ya taifa ya hivi sasa ambayo ni tani 490,000 kwa mwaka.

Kuhusu suala la ubora wa sukari iliyoingizwa nchini, kiongozi huyo alisema ubora wake si wa kutiliwa shaka kwa kuwa ubora wa bidhaa za chakula nchini hudhibitiwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Alisema mtu yeyote anayetaka kujiridhisha ubora na usalama wa sukari iliyoingizwa nchini anaweza kuona nakala za COC na Lab test za TBS.

Kuhusu serikali kupoteza mapato kwa kutoa msamaha wa kodi, alisema lengo la serikali halikuwa kuzinufaisha kampuni zilizoagiza sukari, bali ni kulinda walaji wa mwisho kwa kupunguza makali ya bei ya sukari katika kipindi cha uhaba.

"Ikumbukwe kuwa msamaha huu wa kodi uliombwa na TSPA yenyewe na wanachama wake ambao ni sehemu ya wanufaika," alisema.

Kuhusu madai ya kuwa wenye viwanda vya uzalishaji sukari wana mtindo wa kuhodhi sukari kwa hila na njama ya kuhujumu (Cartel), kiongozi huyo aliitaja ni upotoshaji kwa umma na haina ukweli.

Vilevile, alisema si kweli kwamba sera za nchi katika tasnia ya sukari hazitabiriki kama ambavyo imebainishwa na wazalishaji.

"Serikali ipo tayari kwa majadiliano na wazalishaji kwa maeneo ambayo wanadhani yanakwamisha uwekezaji katika tasnia ya sukari.

"Serikali inasisitiza kuwa mabadiliko yoyote yatakayopendekezwa ni lazima yalenge kulinda maslahi ya wadau; mnyororo wa thamani, kwa maana ya wakulima, wazalishaji na walaji," alisema.

Prof. Bengesi alisema mabadiliko ya sheria yamelenga kuleta ufanisi mkubwa katika sekta hiyo ikiwamo kuhakikisha kunakuwa na uwazi katika mfumo wa usambazaji sukari na nchi wakati wowote inakuwa na hifadhi ya sukari kwa ajili ya dharura.

Kuondoa changamoto zilizopo katika uagizaji sukari ya kuziba pengo, alisema serikali imeona ni vyema kuwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi wa Chakula (NFRA) ambao hauna mgongano wa kimaslahi katika biashara hiyo.

"Hatua hii ni kuhakikisha kuwa sukari kama sehemu ya usalama wa chakula inapatikana wakati wote na kwa bei inayohimilika kwa Mtanzania mwenye kipato cha chini," alisema.

Prof. Bengesi alisema serikali itaendelea kulinda uwekezaji katika tasnia ya sukari kwa maslahi mapana ya nchi kwa kuwalinda wadau wengine wakiwamo wakulima wa miwa, walaji na taasisi za kifedha.

"Serikali iko tayari wakati wote na itaendelea kufanya majadiliano na wadau wote wakiwamo wawekezaji katika tasnia hii ili kupata suluhu ya changamoto zinazowakabili na kutafuta namna bora ya kuzipatia ufumbuzi kwa ajili ya uendelevu wa tasnia ya sukari," alisema.

Prof. Bengesi alisema wamebaini kunapotokea upungufu, bei zinapanda na hazirudi kirahisi kwenye bei za kawaida, hivyo kwa kuipa jukumu NFRA wataondoa tatizo hilo.

Kumekuwa kukiibuliwa hoja mbalimbali kuhusu uingizaji sukari nchini, ikiwamo wakati wa Bunge la Bajeti ambalo Mbunge wa Kisesa, Luhaga Mpina alibuka na tuhuma dhidi ya Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe zilizosababisha mbunge huyo asimamishwe kuhudhuria vikao 15 vya Bunge.

Mwanzoni mwa juma hili, wazalishaji sukari nchini walipoitisha mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam na kueleza yanayojiri katika tasnia hiyo, yakiwamo madai ambayo Bodi ya Sukari iliyatolea ufafanuzi jana.

HABARI KITAIFA

# Samia: Kuna kitu nyuma ya mgomo wa Kariakoo

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema mgomo wa wafanyabiashara wa Soko Kuu la Kimataifa Karikaoo, jijini Dar es Salaam ulikuwa na shinikizo la kisiasa nyuma yake.

Mkuu wa Nchi pia ametaja sababu za kumwondoa Alphayo Kidata katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), akimhamishia ofisini kwake, Ikulu.

Rais Samia alitoa kauli hiyo jana Ikulu ndogo ya Tunguu, Zanzibar baada ya kuwaapisha viongozi wapya alioteua hivi karibuni.

Alimwagiza Waziri mpya wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo kutobaki ofisini, bali awekeze muda wake katika kuleta mapinduzi ya uendeshaji Soko la Kimataifa Kariakoo.

“Ninataka ukaifanye Kariakoo inayotoa huduma saa 24, yenye usalama wa biashara na wafanyabiashara. Kwahiyo, utakaa vipi? Mtajipanga na Jeshi la Polisi, hiyo ni kazi yako.

“Ninataka Kariakoo pawe international market (soko la kimataifa) na kwa sababu mwaka huu tunamaliza yale majengo, machinga wote wataingizwa ndani ya soko,” Rais Samia aliagiza.

Alisema Kariakoo kuna siasa, akieleza kuwa hata wakati wa mgomo ulioitishwa wiki mbili zilizopita, alituma watu kwa siri kwenda kuhoji wafanyabiashara; wengi wao walisema hawajui sababu ya mgomo isipokuwa waliambiwa wagome.

Alisema kuwa mara nyingi changamoto za soko hilo zinatokana na siasa, hivyo akamwelekeza Waziri Jafo akazishughulikie.

Rais alitoa angalizo kwa Dk. Jafo kuwa hataki kusikia wafanyabiashara wanamtafuta waziri, hapatikani kwa kuwa wanatambua kuwa ana uwezo na mdomo wa kuongea katika kumaliza matatizo yao.

Alisema biashara ya hivi sasa si kazi ya ofisini, inahitaji kufanywa kwa vitendo, hivyo ni lazima waziri huyo akubali kwenda nje na kufuatilia ili kujua kinachoendelea.

“Waziri unahitaji kuwa na uhusiano wa karibu sana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji na wizara zinazohusiana ili kuifanya (sekta ya) biashara nchini kuwa vizuri,” aliagiza.

Alielekeza waziri huyo kuhakikisha kila baada ya miezi mitatu anampatia taarifa namna biashara zinavyokwenda nchi nzima kwa kushirikiana na wakuu wa mikoa pamoja na kuwasajili wafanyabiashara wote ili wajulikane.

“Nenda ukawafanye wafanyabiashara kuwa marafiki zako na siyo maadui, kila wanapotaka kukuona fungua milango. Ninataka kukuona ukifanya kazi kwa bidii ili kuifanya Kariakoo kuwa sehemu salama kwa biashara ya kimataifa.

“Nilipokuwa nikifungua Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), nilisema serikali itaendelea kusikiliza na kutatua changamoto zinazokabili wafanyabiashara nchini, hivyo ninahitaji mwende kulisimamia hili vizuri,” aliagiza.

**SIRI YA KIDATA**

Kuhusu Kidata, Rais Samia alisema aliamua kumwondoa Kidata katika nafasi ya Kamishna Mkuu wa TRA baada ya kuona kuwa “mwisho wa siku atadata”.

Alisema Kidata alifanya kazi nzuri katika mamlaka hiyo, lakini ameona nafasi hiyo ichukuliwe na Yusuph Mwenda ambaye alimtambulisha “ni kijana wa Dar es Salaam na mtoto wa mjini, uhuni wote ulioko TRA ameufanya”.



Alphayo Kidata

Alimtaka Kamishna Mkuu mpya Mwenda kwenda kushughulikia mianya yote ili kuhakikisha kila mtu anayestahili kulipa kodi analipa.

“Idadi kubwa ya wafanyabiashara kote nchini hawalipi kodi kwa vile wanakwepa kutumia vifaa vya kielektroniki (EFD), mkapange mipango madhubuti ya kukabiliana na changamoto hiyo,” aliagiza.

Rais alihimiza kupanua wigo wa ulipaji kodi nchini ili serikali isiendelee kukopa, akisisitiza kuwa kukopa kunafedhehesha.

Mkuu wa Nchi alimwagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji kuchukua nishati safi ya kupikia kama ajenda yake ya kipaumbele pamoja na masuala mengine ya mazingira na muungano.

Kuhusu Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Yahya Samamba, Rais Samia alimtaka kwenda kufanya kazi kwa karibu na viongozi wengine ili kufanyia kazi suala la utoaji leseni za uchimbaji madini.

***Imeandaliwa na Romana Mallya (DAR) na Rahma Suleiman (ZNZ)**


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **‘’subscribe’’**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **‘’E-Paper’’** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# THRDC yaanika takwimu matukio ya utekaji

**Christina Mwakangale na Pilly Kigome**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) umetoa angalizo la kutochukuliwa hatua kwa wahusika wa tuhuma za utekaji, huku takwimu zinazobainisha watu 86 walitekwa nchini katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2016-2019.

Umesema watu hao walitekwa na baadhi yao miili ilikuwa imetelekezwa, wengine hawajulikani kama walipona na hakuna watuhumiwa waliokamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mratibu wa mtandao huo, Onsesmo Olengurumwa, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akitoa Ripoti ya Hali ya Watetezi wa Haki za Binadamu na Nafasi ya Kiraia Tanzania Mwaka 2023 kwa wahariri na waandishi wa habari.

"Hii ni Ripoti ya 11 ya Watetezi wa Haki za Binadamu. Kati ya walitekwa kipindi hicho watoto ni 23 na watu wazima ni 63. Matukio ya hivi karibuni ya watu kupotea, kutekwa yanaongezeka kwa watu ambao wanaonekana kuwa na mawazo mbadala. "Hii ni kinyume cha Ibara ya 18 ya Katiba ambayo inampa kila mwananchi haki ya uhuru wa mawazo. Matukio ya utekaji yamekuwa yakichafua taswira ya nchi," alisema Olengurumwa.

Akibainisha baadhi ya matukio hayo, akilitaja la utekwaji mwandishi wa habari Absalom Kibanda, mfanyabiashara Mohamed Dewji, msanii Roma, Sativa pamoja Dk. Steven Ulimboka, hakuna aliyewahi kukamatwa wala ripoti ya uchunguzi iliyotolewa. Olengurumwa alitoa mapendekezo ya kulinda watetezi wa haki za binadamu, wakiwamo waandishi wa habari, akisema serikali ione umuhimu wa kupitisha sera ya watetezi wa haki za binadamu iliyoundwa na mtandao huo na kutunga sheria ya kuwalinda.

Alisema wanapendekeza pia kiundwe chombo maalum cha kufuatilia matukio hayo na kuyachunguza; iwe tume au bodi ambayo itakuwa huru, isiyohusisha taasisi za umma zinazotuhumiwa.

Aliongeza kwamba sheria kandamizi zinazominya uhuru wa vyombo vya habari nchini pia zifanyiwe marekebisho kama vile Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya 2016, Sheria ya Uhalifu wa Mtandao ya Mwaka 2015, Sheria ya Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta ya Mwaka 2010 na Kanuni za Yaliyomo Mtandaoni za Mwaka 2020.

"Tunamwonda Rais aunde tume maalum itakayochunguza sheria za vyombo vya habari nchini, " alisema Olengurumwa.



Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Mrisho Selemani (mwenye kofia nyekundu), akiwaongoza vijana wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), waliotembelea Bandari hiyo, jana, kujionea uwekezaji uliofanywa na Kampuni ya DPW. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TET yataja manufaa mtaala ulioboreshwa

**Na Maulid Mmbaga**

TAASISI ya Elimu Tanzania (TET) imesema muundo wa mtaala mpya ulioboreshwa ni nyumbufu na utampa uwanda mpana mwanafunzi kubobea katika fani mbalimbali zitakazomsaidia baada ya kuhitimu kidato cha nne, sita na chuo kikuu aweze kujiajiri au kuajiriwa.

Imesema kilichoboreshwa zaidi katika mtaala huo ni elimu ya msingi ambayo itatolewa kwa miaka sita, tofauti na saba ya awali, na elimu ya lazima kwa miaka 10 badala ya saba.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam kwenye Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (Sabasaba), Mkuza Mitaala wa TET, Agusta Kayombo, alisema jambo lingine ambalo wanafunzi watanufaika nalo ni kuanzishwa masomo ya Historia ya Tanzania na Maadili.

"Jambo lingine kubwa ni kwamba somo la Kiingereza litaanza kufundishwa kuanzia darasa la kwanza kwa shule zinazotumia lugha ya Kiswahili, vivyo hivyo shule za Kiingereza zitafundisha Lugha ya Taifa kuanzia darasa hilo," alisema Agusta.

Aliongeza kuwa kazi ambayo wamekuwa wakiendelea nayo ni kuandaa vifaa vya mitaala, kutoa mafunzo kwa walimu kazini, kufanya utafiti mbalimbali na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa serikali kuhusu wapi pa kuboresha.

Alisema machapisho wanayoandaa ni pamoja na vitabu vya kiada, kuanzia elimu ya awali mpaka kidato cha sita kwa wanafunzi wa kawaida, wenye uoni hafifu na wasioona kabisa.

Agusta alisema pia wanatoa elimu kuhusu maboresho ya mitaala, akitoa wito kwa wananchi kutembelea banda lao katika viwanja vya Sabasaba ili waweze kuongezwa uelewa zaidi na kupatiwa machapisho kwa ajili ya watoto wao.

# Uwekezaji katika Bandari Dar waduwaza viongozi UVCCM

**Na Joseph Mwendapole**

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) umetembelea maeneo ya uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam uliofanywa na kampuni ya DP World na kusema uwekezaji huo umeleta mabadiliko makubwa ya kiutendaji na ufanisi.

Akizungumza baada ya kuzuru katika Bandari ya Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Taifa wa UVCCM, Mohamed Kawaida alipongeza serikali kwa uamuzi wake wa kuruhusu uwekezaji huo ambao alisema una manufaa makubwa kwa taifa.

Alisema ripoti ya utendaji iliyowasilishwa na uongozi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) umeonesha kuongezeka kwa ufanisi na kazi ya upakuaji na usafirishaji mizigo bandarini huko tofauti na hofu iliyokuwapo awali na watu waliokuwa wanapinga uwekezaji huo.

"Sisi ni wasimamizi wa serikali katika utekelezaji Ilani ya CCM, tumeamua kutembelea Bandari ya Dar es Salaam kujionea shughuli mbalimbali zinavyofanyika na tumefurahishwa na ufanisi wake baada ya uwekezaji mkubwa," alisema Kawaida.

Alisema kuwa lengo kuu la ziara hiyo iliyohusisha pia wenyeviti na makatibu wa umoja wa vijana kutoka mikoa yote nchini, ni kujionea na kujifunza namna kazi zinavyofanyika bandarini huko.

"Mimi na viongozi wenzangu wote wa UVCCM tumefurahishwa na tija ya uwekezaji huu katika Bandari ya Dar es Salaam.

"Awali kulikuwa na maneno mengi ya upotoshaji kuwa uwekezaji huo hauna tija kwa taifa na Watanzania wengi wangepoteza ajira na wafanyabiashara kukimbilia bandari nyingine za nchi jirani," alisema.

Kiongozi huyo wa UVCCM alisema mwekezaji DP World amewekeza fedha nyingi katika miundombinu na vitendea kazi, hali ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka shehena za mizigo katika bandari hiyo.

"Lakini katika ziara hii tumejionea hali tofauti kabisa, ufanisi wa upakuaji mizigo umeongezeka baada ya uwekezaji mkubwa wa miundombinu na vitendea kazi kufanyika.

"Hii inamaanisha kuwa mapato yanayotokana na uwekezaji huu yameongezeka na kuwa na tija katika maendeleo ya nchi yetu," alisema Kawaida na kuongeza kuwa Tanzania imepata neema ya kuwa na bandari hiyo inayohudumia nchi mbalimbali zikiwamo Rwanda, Burundi, Congo DRC, Msumbiji na Zambia.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa TPA, Plasduce Mbosaa, Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Mrisho Selemani, alisema viongozi wa umoja huo wamefurahishwa na ufanisi unaofanywa na mwekezaji DP World bandarini huko kama ilivyotarajiwa na wamejifunza mengi wakati wa ziara hiyo.

Alisema ili kuleta ufanisi na tija, mwekezaji DP World ameweka vitendea kazi mbalimbali bandarini huko katika kuhudumia shehena za mizigo na kufanya ufuaji wa mashine zilizokaa muda mrefu bila kufanya kazi.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi kuendelea kuitumia bandari hiyo kutokana na mageuzi makubwa yanayofanyika katika kuharakisha kazi ya upakiaji na upakuaji mizigo bandarini huko.

Ripoti ya utendaji kazi wa bandari hiyo iliyowasilishwa wakati wa ziara hiyo kwa viongozi wa umoja huo, imeonesha mafanikio makubwa yamepatikana baada ya serikali kuridhia uwekezaji wa DP World bandarini huko.

Ripoti hiyo imeonesha kuwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita (2020-2023), mapato ya Bandari ya Dar es Salaam yamekuwa yakiongezeka kwa wastani wa asilimia 27.2 kwa mwaka, kutoka kiasi cha Sh. bilioni 801.7 hadi trilioni 1.3 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kulikotokana na kuongezeka kwa shehena zikiwamo kutoka nchi za jirani.



Mafundi wakijenga chemba ya maji taka na ya mvua yanayoelekea baharini katika eneo la Buguruni jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# RC Mtanda alia na usitishwaji holela safari za ndege za ATCL

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda amelalamikia tatizo la usitishwaji holela safari za Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ambao umekuwa unajitokeza mara kwa mara bila kuwapo taarifa maalum kwa wateja.

Kufuatia hali hiyo, Mtanda ameitaka ATCL kubadili hali ya utoaji huduma kwa wateja hasa kunapokuwa na dharura za namna hiyo ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa mapema na kuona namna ya kufidishia hasara wanazoingia wateja wao.

Mtanda alitoa kauli hiyo juzi jijini hapa wakati wa utiaji saini mkataba wa ushirikiano baina ya ATCL na kampuni ya utoaji huduma kwa wateja ya Via Aviation kwa aajili ya kuhudumia wasafiri wa daraja ya biashara kupitia jengo lake la Serengeti Lounge lililoko katika Uwanja wa Ndege Mwanza.

Alisema safari zimekuwa zikisitishwa huku wateja mara kwa mara wakitakiwa kusubiri na baadaye kuambiwa safari imeahirishwa, hali aliyoitaja kuwapa wakati mgumu viongozi wa serikali. Alisema hali ya dharura mara nyingi zinakuwapo hata katika mataifa yaliyoendelea, lakini wao wanakuwa na ukarimu kwa wateja wao hadi kuwasahaulisha usumbufu waliokutana nao, tofauti na kinachojiri kwa safari za ATCL.

"Mara nyingi hali hizi zikitokea viongozi ndio tunatafutwa, pengine wakijua sisi ndio tuna suluhisho la matatizo kama hayo, lakini pengine unakuta hata sisi wenyewe tunakutana na kero kama hiyo tukihitaji kusafiri, hivyo mjitahidi pale mnapokuwa na dharura toeni taarifa zinazoeleweka kwa wateja.

"Kingine lazima jiji la pili kwa ukubwa na la kimkakati nchini liwe limeunganishwa na makao makuu ya nchi, nina imani ATCL mtafanya mchakato wa kurejesha safari za Mwanza-Dodoma haraka kwani hili si takwa la kisiasa, bali ni kwa maslahi makubwa ya nchi na shirika lenyewe," alisema Mtanda.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Ladislaus Matindi alisema kuwa katika kukabiliana na kero hiyo, shirika hilo linaendelea na maboresho ambapo Julai 14 mwaka huu, wanatarajia kupokea ndege mpya aina ya Boeing 787-800.

Alisema ndege hiyo yenye uwezo wa kubeba abiria 181 itaongeza nguvu kwa ndege zilizopo ikiwa ni pamoja na kurejesha haraka iwezekanavyo safari za moja kwa moja kutoka Mwanza hadi Dodoma ili kuondoa usumbufu wa kuzunguka Dar es Salaam.

"Kuingia mkataba na Via Aviation kupitia huduma zao katika jengo la Serengeti Lounge ni sehemu ya kumjali mteja wetu wa daraja la biashara ambaye atapata huduma muhimu bila malipo katika jengo hilo," alisema.

Akizungumza ya kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Via Aviation, Susan Mashibe, Mkuu wa Usimamizi na Uendelevu wa kampuni hiyo, Caleb Takayindisa alisema lengo la kuanzisha huduma hiyo ni kuboresha viwango vya ubora wa usafirishaji katika viwanja vya ndage nchini.

# Bilioni 81/- zatumika miradi ya BOOST

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SHILINGI bilioni 81.297 zimetumika kukamilisha ujenzi wa shule mpya 78 na kuboresha miundombinu mbalimbali ya shule katika kutekeleza programu ya BOOST kwa mwaka 2023/24.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo alibainisha hayo jana katika hotuba yake iliyosomwa na Kamishna wa Elimu, Dk. Lyambwene Mutahabwa wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kwa walimu wakuu na maofisa mazingira kuhusu ujenzi wa miundombinu ya shule kupitia Programu ya BOOST yanayofanyika mjini Morogoro. Prof. Nombo alitaja miundombinu iliyojengwa kuwa ni pamoja na vyumba vya madarasa 1,625, matundu ya vyoo 3,635, nyumba za walimu 10 na ukarabati wa shule 42.

Alisema kuwa kwa mwaka 2022/23, serikali ilijenga shule mpya za msingi 302, vyumba vya madarasa 7,230 na matundu ya vyoo 11,297.

Alisema serikali imeamua kufanya hivyo kupitia mradi wa BOOST unaosaidia masuala ya kuboresha elimu bure shuleni ambapo ujenzi wa miundombinu hiyo utasaidia kukabiliana na changamoto ya msongamano wa wanafunzi madarasani uliotokana na mwitikio mkubwa wa uandikishaji watoto kuanzia shule za awali.

Alielekeza washiriki hao kushiriki kikamilifu mafunzo hayo ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji miongozo ya ujenzi, taratibu za ununuzi na matumizi ya mfumo wa NeST katika ununizi wa ngazi ya shule, usimamizi wa fedha na bajeti na usalama wa mazingira na jamii.

Pia aliagiza walimu wakuu wa shule za msingi nchini kuhakikisha wanaweka mifumo na mikakati thabiti ya kulinda watoto dhidi ya unyanyasaji na ukatili wa aina yoyote ili kufanya shule kuwa mazingira salama kwao.

Ofisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Paulina Mkwama aliwataka walimu kuhakikisha wanawapa ujuzi watoto huku wakiwalea kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi yao vinavyoripotiwa kwa wingi hivi sasa nchini.

Alisema kama walimu wakisimamia vyema masuala ya ujuzi na kulea watoto, wataokoa vitu vingi ikiwamo usimamizi mzuri wa mazingira, maadili na maendeleo katika jamii.

Mratibu Programu ya BOOST, Ally Swalehe alisema programu hiyo ya miaka mitano ilioanza mwaka 2021/22 na kutarajiwa kukamilika mwaka 2025/26, inatekelezwa katika halmashauri zote 184 za Tanzania Bara kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kwa mkopo wa Sh. trilioni 1.5, ikilenga kuboresha elimu kuanzia ngazi ya awali.

Alisema program hiyo inajumuisha afua 8 za kielimu ikiwamo kuboresha miundombinu ya shule na ufundishaji na ujifunzaji kitaalamu ili kusaidia mtoto, akifika darasa la pili anakuwa anajua kusoma na kuandika na kuondoa changamoto ya kuwa na wanafunzi wasiojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) shuleni.

Mshiriki wa mafunzo hayo, Daudi Mlahagwa, Ofisa Mazingira kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Pangani mkoani Tanga, alisema yatasaidia kutekeleza miradi inayogusa jamii ili kupiga hatua katika maendeleo.

Naye Mkuu wa Shule ye Msingi Mzalendo, Manispaa ya Moshi, Pascal Shirima alishukuru serikali kwa kuwapatia mafunzo ambayo anamini yatasaidia kuwaongezea uzoefu katika masuala ya miradi na kuondoa dosari ndongo wanazokumbana nazo wakati wa utekelezaji miradi hiyo.

# "Watoto msikae kimya mnapofanyiwa ukatili'

**Na Maulid Mmbaga**

OFISA Ustawi wa Jamii Wilaya ya Mkuranga, Amina Aloyce, amesisitiza wanafunzi katika wilaya hiyo pamoja na Tanzania kwa ujumla kutoficha matukio ya ukatili wa kijinsia wanayofanyiwa kwa kuwa watasababisha tatizo hilo kukua badala ya kukomeshwa.

Alitoa rai hiyo jana wilayani Mkuranga, mkoani Pwani, wakati Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation (AMF) ilipokuwa ikigawa msaada wa taulo za kike kwa wanafunzi 842 wa Shule ya Sekondari Ali Hassan Mwinyi.

Alisema kumekuwa na aina zaidi ya tatu za ukatili wa kijinsia ambazo watoto kwa ujumla wamekuwa wakifanyiwa katika mazingira tofauti, lakini kumekuwa na tatizo kwa baadhi yao kushindwa kuyawasilisha kwa walezi wao baada ya kufanyiwa.

"Tunaomba wazazi, wananchi na wanahabari waendelee kutusaidia kupaza sauti katika kukemea ukatili dhidi ya watoto wetu, kila mmoja ajue kuwa ana jukumu la kumlinda mtoto," alisisitiza Amina.

Mkurugenzi wa AMF, Asma Mwinyi, alisema dhumuni la kutoa taulo hizo ni kumwezesha mwanafunzi kuwa na furaha na kuendelea kuhudhuria darasani pasipo kuwa na shaka yoyote, hasa akiwa kipindi cha hedhi, ikiwa ni mwendelezo wa kampeni yake ya "Nisitiri Nisifedheheke'.

"Jitihada hizi kwa kiasi kikubwa ni ili kuunga mkono mkakati wa serikali katika kutoa elimu bora kwa wanafunzi bila kukutana na changamoto yoyote inayoweza kuwafanya washindwe kuhudhurua masomo yao," alisema Asma.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Mkuranga, Omary Mwanga, alisema jitihada hizo zinafanywa kwa kuzingatia umuhimu wa wanawake, na kwamba hiyo ni katika kuwatengenezea mazingira mazuri watoto kwa mustakabali wa maendeleo yao, jamii na taifa.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga, Azam, Coastal acheni mazoea kuelekea CAF

**MSIMU** mpya wa mashindano ya kimataifa Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika unatarajiwa kufanyika kuanzia Agosti 13, mwaka huu.

Mashindano hayo yanaandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), hufanyika kila mwaka na baadhi ya timu huanzia katika hatua ya awali, huku nyingine zikisubiri raundi ya kwanza.

Tanzania Bara katika mashindano hayo itawakilishwa na timu nne, mabingwa wa Ligi Kuu, Yanga na Azam FC wao watashiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku Simba na Coastal Union zenyewe zitapeperusha bendera ya nchi kwenye mashindano Kombe la Shirikisho.

Kwa upande wa Zanzibar, JKU SC itakiwakilisha kisiwa hicho katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Chipukizi ya Pemba wao wamepata nafasi ya kushiriki kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho baada ya kuibuka mabingwa wa Kombe la ZFF Cup (Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar).

Maandalizi mazuri yanaanzia katika kusajili wachezaji wenye ubora ambao unafanana na ukubwa wa mashindano hayo ya CAF, ambayo hufanyika kila mwaka na washindi kujizolea zawadi nono ya fedha zinazotolewa na shirikisho hilo linalosimamia nchi wanachama 54.

Timu zote zilizopata tiketi ya kushiriki mashindano hayo ya kimataifa, zinatakiwa kuboresha vikosi vyake kwa kuzingatia ripoti ya kiufundi iliyowasilishwa na makocha wa timu husika.

Klabu inayofanya usajili kwa kufuata mapendekezo ya benchi la ufundi, ina nafasi kubwa ya kufanya vizuri katika mashindano yote itakayoshiriki huku ile ambayo bado inajiendesha 'kizamani' kwa viongozi kuchukua jukumu la kusimamia usajili.

Umefika wakati kila mtu ndani ya klabu akafanya majukumu yake ili kuhakikisha matokeo chanya yanapatikana baada ya kuanza kwa msimu mpya wa mashindano ambao husubiriwa kwa shauku na mashabiki na wanachama wao.

Viongozi wa timu zilizofuzu kushiriki mashindano hayo ya CAF waache kujiendesha kwa mazoea, soka la sasa linahitaji kusimamiwa kwa kufuata misingi sahihi, kuendesha klabu kwa weledi husaidia na hurahisisha timu kufanya vizuri katika michuano yote itakayoshiriki.

Lakini kabla ya kushiriki mashindano, viongozi wanatakiwa kufanyia kazi ripoti za makocha katika kusajili wachezaji, waachane na usajili wa kukomoana ambao mwisho wa msimu, ni klabu husika ndio huingia hasara kwa kupoteza nguvu kazi na rasilimali fedha mahali ambapo hawakustahili kufanya hivyo.

Jambo lingine muhimu ni klabu zinatakiwa kuweka kambi katika sehemu ambayo itawasaidia wachezaji kufuata vyema programu za makocha wao na kuacha tabia ya kukimbilia kuweka kambi kwenye maeneo ambayo hayafanani na hualisia mahali klabu husika itatumia muda mrefu kucheza mechi zake za ligi au mashindano ya kimataifa.

Klabu pia zinatakiwa kuwaandaa wachezaji kudumisha nidhamu ndani na nje ya uwanja, wawaeleze wachezaji nidhamu bora husaidia kunyanyua viwango vyao kwa sababu wakati wote watakuwa wanafanya mambo ambayo hayaendi kinyume na mwongozo unaowahusu.

Tunazikumbusha timu kucheza mechi za kirafiki zitakazowasaidia kuwajenga wachezaji na kuacha kutafuta michezo dhidi ya timu dhaifu ambazo huzifunga idadi kubwa ya mabao na kushangilia huku ikiwakwepa vigogo wenzao ambao ndio wanastahili kujipima nao na kufanya tathmini sahihi ya mazoezi waliyofanya ya 'Pre- Season'.

Huu ndio wakati wa kila timu kufanya maandalizi na kuacha kutoa visingizio pale msimu mpya utakapoanza kwa kujitetea wachezaji bado hawajazoea mfumo au bado timu haina muunganiko.

Tunazitakia kila la kheri timu zote 16 zitakazoshiriki Ligi Kuu Bara, Ligi ya Championship (zamani Ligi Daraja la Kwanza), First League (Ligi Daraja la Pili), Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL) na mashindano mengine yote yatakayofanyika hapa nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Waliomshambulia Mo Dewji wako wapi kipindi cha usajili?

**HIKI** ni kipindi cha usajili, klabu mbalimbali ndani na nje ya Tanzania, ikiwamo Simba SC zinafanya usajili kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyao ili viwe imara kuelekea msimu ujao.

Simba inaonekana kufanya usajili mkubwa ili kupambana kurejesha heshima ya klabu hiyo iliyopotea kwa misimu mitatu mfululizo iliyopita.

Kwa jicho la tatu tu, inaonekana inawaondoa baadhi ya wachezaji wenye umri mkubwa na waliokaa muda mrefu klabuni, ikisajili vijana zaidi.

Kwa asilimia zaidi ya 90, anayefanya usajili katika klabu hiyo ni Mwekezaji, Rais wa Heshima na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mohamed Dewji 'Mo Dewji'.

Kipindi hiki cha usajili wala hatusikii watu wakimpigia kelele aache kusajili ili zoezi hili lifanywe nao.

Hatusikii hata mmoja kumpa moyo au kumwambia watamsaidia kusajili hata wachezaji wawili tu.

Badala yake usajili unaofanywa atatoa pesa kama mwekezaji ambaye anawekeza kwenye biashara zake akitegemea kupata faida baadaye.

Kuna baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba ambao hivi karibuni walionekana kuchachamaa, wakimtaka Mo awaachie timu yao kwa sababu hana lolote analofanya.

Baadhi yao wakaenda mbali zaidi na kusema ananufaika na klabu hiyo kuliko klabu inavyonufaika naye.

Wapo waliomtaka aondoke kwa sababu eti wamepata wawekezaji wengine ambao wana fedha nyingi au watawekeza zaidi kuliko yeye.

Sasa kuna wale ambao walikuwa wanasema ni mbahili hatoi fedha ndiyo maana timu haijafanya vizuri kwa misimu hii yote mitatu.

Kusema kweli Mo alipata mashambulizi mengi mara baada ya Ligi Kuu kumalizika, ambapo baadhi ya watu walimjia juu kila mmoja akipeleka shutuma kwake.

Hata hivyo ukiangalia kwa jicho la tatu tu, utagundua inawezekana kulikuwa na ajenda maalum, au hasira ya baadhi ya wanachama na mashabiki kwa kukosa ubingwa, huku kikosi kikionekana kimechoka, lakini si kweli hatoi pesa.

Mo ndiye mwekezaji na kazi yake ilikuwa ni kutoa pesa na viongozi waliopo madarakani ndiyo walikuwa na kazi ya kusaka wachezaji wazuri, lakini hawakufanya hivyo.

Ukitaka kugundua hili, kipindi chote hiki hakukuwa na shida ya mishahara ya wachezaji, kuanzia ya wakubwa, wanawake, vijana chini ya miaka 20, hadi 17. Shida kubwa ilikuwa ni usajili wa wachezaji wasiokuwa na viwango.

Sasa mwenyewe ameamua kufanya usajili, akitengeneza kikosi chake kidogo anachokiamini na kutoa fedha kwa ajili ya usajili ili yasijirudie tena.

Na kweli, tayari ameanza kuwasajili Joshua Mutale, Steven Mukwala, Jean Charles Ahoua, Abdulrazack Hamza, Valentino Mashaka na wengineo na anaendelea.

Niliteg emea kipindi hiki wale ambao walikuwa wanamkosoa kuwa mfanyabiashara huyo hatoi fedha ya usajili, na waliokuwa wanataka aondoke angalau tu wamsaidie kuleta wachezaji ili kuisaidia Simba na yeye mwenyewe kumpunguzia mzigo.

Hatusikii basi hata anayejitokeza awalipe hata jopo la makocha, badala yake wapo kimya kama hawapo.

Nadhani wanasubiri ligi ianze ifanye vibaya ndiyo wajitokeze tena. Binafsi nawaambia wanachama na mashabiki wa Simba soka la sasa linahitaji fedha nyingi, si kama la zamani.

Wale wanaosema atuachie timu yetu, sidhani kama wanaweza kumlipa mshahara kocha hata mmoja tu.

Siku hizi hata benchi la ufundi lina makocha wengi tofauti na zamani, ambapo mbali na kocha mkuu na msaidizi, mwalimu wa makipa, kuna mtaalam wa chakula, utimamu wa mwili, daktari, na hata watathmini wa timu pinzani.

Hawa wote wanahitaji mishahara pia, achilia mbali wachezaji. Wakati mwingine tuheshimu matajiri hawa tu wachache ambao wameamua kuwekeza kwenye soka kwa sababu si wengi wenye mapenzi na mchezo huu.

Nikikumbuka 'povu' la watu kwa Mo, na sasa wamemwachia mwenyewe atoe fedha za usajili, napatwa mshangao kwa sababu nilidhani na wao wanaweza kufanya hivyo hata kidogo tu kwa kuisaidia Simba ambayo wanaonekana kama wanaipenda sana kuliko mwekezaji mwenyewe.

## HABARI KITAIFA

# Jela kwa kumkata viganja mama mdogo

**Na Daniel Limbe,** CHATO

MAHAKAMA ya Wilaya ya Chato, mkoani Geita imemhukumu Faida Enocka kutumikia kifungo cha miaka minne gerezani na kulipa fidia ya Sh. milioni tatu baada ya kupatikana na hatia ya kumkata viganja vya mikono mama yake mdogo, Monica Nengo na kumsababishia ulemavu wa kudumu kutokana na imani za kishirikina.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Erick Kagimbo baada ya kusikiliza maelezo na ushahidi wa pande zote mbili uliowasilishwa mbele ya mahakama hiyo.

Katika kesi hiyo namba 757 ya mwaka 2023, Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Mwendesha Mashtaka wa Polisi Mauzi Lyawatwa.

Mwendesha Mashtaka huyo alidai mahakamani huko kuwa mnamo Julai 20, 2022, saa mbili usiku, mshtakiwa alimshambulia mama yake mdogo kwa kitu chenye ncha kali kutokana na imani za kishirikina kisha kumsababishia ulemavu wa kudumu.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo alidaiwa kuwa baada ya kutambua kuwa ametenda ukatili, alikimbia kwenda kujificha kwa lengo kukwepa mkono wa sheria na baada ya kukamatwa na Jeshi la Polisi, alifikishwa mahakamani Oktoba 26, 2023.

Lyawatwa alidai kuwa kitendo hicho cha kujeruhi ni kinyume cha kifungu namba 225 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, kama kilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022, huku akiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa.

Licha ya mshtakiwa huyo kukana kosa mbele ya mahakama hiyo, mahakama hiyo ilimkuta na kesi ya kujibu.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea ili kupunguziwa adhabu, akidai kuwa ana watoto pamoja na mama yake mzazi wanaomtegemea na kwamba kwa kuzingatia kuwa amekaa gerezani muda mrefu, mahakama imwonee huruma.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Kagimbo alisema kuwa kutokana na ushahidi uliowasilishwa na Upande wa Mashtaka na kwa kuzingatia utetezi wa mshtakiwa, mahakama hiyo imejiridhisha pasi na shaka kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo kinyume cha sheria za nchi.

Na kwa kuzingatia utetezi wa mshtakiwa huyo, hakimu huyo alisema mahakama hiyo inamhukumu kifungo cha miaka minne gerezani. Baada ya kumaliza adhabu hiyo gerezani, atatakiwa kumlipa Monica fidia ya Sh. milioni tatu ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hizo.

Mshtakiwa alipelekwa Gereza la Wilaya ya Chato kuanza kutumikia adhabu yake.



Monica Laurent Nengo, akionyesha ulemavu alioupata baada ya kukatwa viganja vya mikono yake. **PICHA: DANIEL LIMBE**

# Babu mbaroni tuhuma kunajisi mtoto mdogo mwenye ulemavu

**Na Allan Isack,** BABATI

JESHI la Polisi mkoani Manyara linamshikilia mkazi wa Kijiji cha Kiru wilayani Babati, Mohamed Omary, kwa madai ya kunajisi mtoto mwenye ulemavu wa miguu (11).

Akizungumza jana na waandishi wa habari mjini hapa, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) George Katabazi, alisema tukio hilo lilitokea Julai 2 mwaka huu katika Kijiji cha Kiru.

Kamanda Katabazi alisema kuwa mzee huyo mwenye umri wa miaka 70 andaiwa kufanya tukio hilo la kikatili akiwa nje ya nyumba anakoishi mtoto huyo.

Alisema kuwa timu ya uchunguzi iko katika eneo hilo kufanya upelelezi ili kubaini sababu ya ukatili huo uliofanywa dhidi ya mtoto huyo.

"Tunaendelea na upelelezi wa tukio hilo la mzee huyu kudaiwa kunajisi mtoto huyo mwenye ulemavu kabla ya kumfikisha mahakamani pindi ukikamilika," alisema Kamanda Katabazi.

Baadhi ya wakazi wa Mji wa Babati wameeleza kusikitishwa na tukio hilo linalodaiwa kutendwa si tu kwa mtoto, bali pia mtoto mwenye ulemavu.

Mkazi wa Kijiji cha Kiru, Jack Haimu, alisema kuwa watu wengi wamesikitishwa na tukio hilo la kikatili.

"Wakazi wengi wa hapa Kiru hawakuwa mbali kutoa hisia zao kuhusu tukio hili, kama ikithibitika mzee huyo achukuliwe hatua kali za kisheria," alisema Haimu.

Mkazi mwingine wa Kijiji cha Kiru, Mwanaidi Ramadhan, alisema tukio hilo ni la kulaaniwa kwa kuwa ni ukatili mkubwa kutenda vitendo vya aina hiyo dhidi ya watoto.

"Huyu mzee sijui kama ni kweli, anatoa fundisho gani kwa watu wa eneo hili hasa vijana na watoto, kwa kuwa hakuna sababu ya msingi ya kumfanyia tukio hilo mtoto huyo," alisema.

Aliomba serikali kuchukua hatua kali dhidi ya mzee huyo kama ikithibitika, ili iwe funzo kwa watu wengine wenye tabia ya kutenda ukatili kama huo.

Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, Kifungu cha 131, kama ikithibitika mzee huyo ametenda kosa hilo, adhabu yake ni kifungo cha miaka 30 gerezani.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed





Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Moses Kusiluka akipata maelezo alipotembelea banda la Wizara ya Kilimo, katika maonyesho ya 48 ya biashara ya kimataifa Dar es Salaam, kwenye uwanja wa Mwalimu Nyerere, barabara ya Kilwa jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mfamasia auawa, mwili watelekezwa barabarani

**Na Moses Ng'wat,** MBOZI

MFAMASIA wa Kituo cha Afya cha Isansa, wilayani Mbozi, mkoani Songwe, Daudi Kwibuja (30), amefariki dunia katika mazingira ya kutatanisha huku mwili wake ukiwa umetupwa kando ya barabara Kuu ya Mbeya -Tunduma katika eneo la Mlowo.

Mwili wa mfamasia huyo ambaye ni mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi katika Idara ya Afya, umekutwa ukiwa na majereha sehemu mbalimbali.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Agostino Senga, alisema juzi kuwa uchunguzi wa awali unaonesha mtumishi huyo aliuawa usiku wa Julai 3, 2024.

Alisema pamoja na awali kudhaniwa kuwa alifariki dunia baada ya kugongwa na gari, lakini baada uchunguzi umebaini alikutwa na majeraha ambayo hayafanani na ya ajali ya kugongwa na gari.

"Uchunguzi unaendelea ili kubaini ni ajali kweli au mauaji kwa hiyo tunaendelea kuchunguza na tutakapopata ukweli kupitia matabibu tutauhabarisha umma chanzo cha kifo cha ndugu yetu huyu (marehemu) kimetokana na nini," alifafanua.

Kamanda Senga alisema baada ya chunguzi kukamalika na wahusika kubainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

# NMB yakabidhi samani za sekondari

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE mbili za mkoani Dar es Salaam zimekabidhiwa meza 90 na viti 90 venye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 10.

Msaada huo umetolewa na Benki ya NMB kwa Shule za Sekondari Uhamiaji, wilayani Temeke na Mchikichini ya wilayani Ilala ikiwa ni utekelezaji azma ya benki hiyo kuboresha ya elimu.

Samani hizo zinatajwa zitapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la upungufu wa samani kwa walimu na wanafunzi na ni sehemu ya utekelezaji Mkakati wa Uwekezaji kwa Kijamii (CSI) unaolenga kusaidia jamii ambayo benki hiyo inafanya kazi.

Katika hafla ya kukabidhi meza na viti hivyo juzi, Kaimu Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Ferdinand Mpona alisema uboreshaji sekta ya elimu ni miongoni mwa vipaumbele muhimu kwa benki yake huku alisisitiza dhamira ya benki hiyo kuendelea kufanya kazi kwa karibu na wadau wote ikiwamo serikali katika kuinua maendeleo ya sekta ya elimu nchini kote.

"Kama benki, tunatambua kuwa elimu ndiyo ufunguo wa maisha ndiyo maana kwa miaka mingi tumewekeza kwa kiasi kikubwa katika kuinua ukuaji wa sekta ya elimu.

"Kwa hakika, sekta ya elimu ni moja ya maeneo ya kipaumbele katika mkakati wetu wa CSI. Tumekuwa tukitenga asilimia moja ya Faida Baada ya Kodi (PAT) kila mwaka ili kuchangia mipango mbalimbali ya maendeleo," alisema.

Mpona aliongeza, "Tunaamini samani tunazotoa leo (juzi) zitasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu."

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, alipongeza benki hiyo kwa ukarimu wake na kusisitiza dhamira ya serikali kuendeleza maendeleo ya sekta ya elimu.

"Tunafahamu kuwa shule nyingi za Wilaya ya Temeke bado zinakabiliwa na changamoto nyingi na zinahitaji msaada zaidi kutoka kwa wadau wa elimu kwa kuwa tuna bajeti ndogo.

"Ninaishukuru Benki ya NMB kwa kuunga mkono jambo hili zuri na ninachukua fursa hii kutoa wito kwa wadau wengine wa ushirika kuungana na azma yetu ya kusaidia maendeleo ya sekta ya elimu," Mapunda alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo wakati wa hafla ya kukabidhi meza 50 na viti 50 vilivyotolewa na Benki ya NMB kwa Shule ya Sekondari Mchikichini, alishukuru benki hiyo kwa kuendelea kuunga juhudi za serikali za kuboresha sekta ya elimu.

"Tunajisikia faraja kwa benki yetu kuendelea kuwa karibu na wananchi. Serikali imeshaleta fedha za kujenga ghorofa katika shule hii ya Mchikichini na matundu ya vyoo.

"Kitendo cha Benki ya NMB kutoa meza na vitu ni jitihada njema za kuunga mkono serikali na siku zote wamekuwa wakituunga mkono kwa vitendo," alisema.

Awali Mkuu wa Shule ya Sekondari Uhamiaji, Christopher Mtabutu alibainisha kuwa shule yake ilikuwa inakabiliwa na upungufu mkubwa wa viti na meza za walimu, akionesha matumaini kuwa samani zilizotolewa na Benki ya NMB kwa kiasi kikubwa zitasaidia kukabiliana na upungufu huo.

"Mchango huu umekuja wakati mwafaka kwani tumekuwa tukikabiliwa na upungufu wa samani kwa ajili ya walimu.

"Ninaamini kuwa madawati na meza ambazo Benki ya NMB imetupatia leo vitasaidia kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu mbali na kuboresha usalama wa mali zao pia," alisema.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Mchikichini, Nelson Nestory alisema, "Msaada wa meza 50 na viti 50 utasaidia sana. Kabla ya kuomba msaada huu tulikuwa na upungufu wa meza na viti 150 na meza 50 ambapo Mkurugenzi alituletea viti 100 na meza 100.

Tukawa na upungufu wa meza 50 na viti 50. Tunaishukuri Benki ya NMB kwa kutupatia meza 50 na viti 50 na kwa sasa tumemaliza tatizo la wanafunzi kukosa meza na viti," alisifu.

Mwalimu huyo aliahidi shule yake kuendelea kutunza vifaa hivyo ili kusaidia vizazi vijavyo.

# NIDA yaanza kuchapisha upya vitambulisho vilivyoharibika

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imeanza kuchapisha upya vitambulisho vilivyochapishwa chini ya ubora na kugawiwa kwa wananchi .

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Mamlaka hiyo, Geofrey Tengeneza, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi kuwa wamekuwa wanapokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa mikoa mbalimbali kuhusu ubora hafifu wa baadhi ya vitambulisho hivyo.

"Tumekuwa tukipokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi wa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Dar es Salaam na mingine kuwa vitambulisho walivyopewa vimefutika picha na majina," alisema.

Baada ya kufanya utafiti na kubaini ukweli juu ya kuwapo changamoto hiyo, ofisa huyo alisema NIDA imeamua kuvikusanya vitambulisho hivyo kutoka kwa wananchi ili kuvichapisha upya.

"Ninapenda kuchukua nafasi hii kuujulisha umma wa Watanzania kwamba mwananchi yeyote mwenye kitambulisho kilichofutika picha na maandishi, akirejeshe kwenye ofisi za kata yake, au ofisi za NIDA zilizopo karibu naye ili achapishiwe na kupewa kitambulisho kipya ndani ya muda mfupi," alisema.

Aliongeza kuwa mamlaka imejipanga kuhakikisha zoezi hilo linafanyika kwa weledi na ubora ili kuhakikisha wananchi husika wanapata vitambulisho vyao ndani ya muda wa wiki mbili pekee.

"Ili kwenda na kasi kubwa ya uhitaji wa vitambulisho vya taifa kwa wananchi, tulilazimika kuchapisha vitambulisho vingi sana ndani ya muda mfupi, zoezi kubwa ambalo lilisababisha baadhi ya vitambulisho kuchapishwa chini ya kiwango kinachotakiwa," alisema Tengeneza.

Alisema kuwa hadi sasa NIDA imefanikiwa kuchapisha na kutoka vitambulisho kwa idadi kubwa; kazi inaendelea kuwafikia wananchi wachache waliosalia.

"Kimsingi, takwimu zetu zinaonyesha kuwa kila Mtanzania aliyeomba kupatiwa kitambulisho cha uraia na aliyekidhi vigezo vilivyowekwa na serikali ameshachapishiwa kitambulisho chake," alisema.

"Changamoto iliyopo hivi sasa ni kwamba watu wengi, hususan mijini hawajakwenda kuchukua vitambulisho vyao, hali ambayo inasababisha kuwa na vitambulisho vingi vituoni," alisema.



## Umri wanaotibiwa kuachana na dawa za kulevya washtua

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KAMISHNA Msaidizi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya Kanda ya Kati, Mzee Kasuwi amesema zaidi ya asilimia 70 ya watu wanaopata huduma za tiba saidizi kutokana na madhara ya matumizi ya dawa za kulevya nchini ni vijana walio chini ya miaka 35.

Amesema kuwa kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, asilimia 34 ya wananchi ni vijana walio chini ya umri wa miaka 35 ambao ndiyo waathirika wakubwa wa dawa hizo, ndiyo tegemeo la taifa.

Kasuwi aliyasema hayo alipozungumza na vijana kuhusu ushiriki wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya wakati wa kongamano lililofanyika Dodoma juzi.

Katika kongamano hilo lililojumuisha vijana zaidi ya 2,500, Kasuwi alisema kuwa hali hiyo inaonesha namna nguvu kubwa inatakiwa kuwekezwa katika kusaidia vijana kutojiingiza katika janga hilo linalopotenza nguvukazi.

Alisema waathirika walio wengi katika kundi hilo ni vijana ambao afya yao imeathiriwa na matumizi ya dawa kulevya na unywaji pombe wa kupindukia, hivyo ni muhimu wakajilinda dhidi ya ulevi huo.

Alisema vijana kushiriki mapambano hayo dhidi ya dawa za kulevya ni muhimu kwa kuwa wao ndiyo waathirika wakubwa wa biashara hiyo haramu na ndiyo washiriki wakuu na matumizi ya mihadarati na dawa zingine za kulevya.

Aliwataka vijana hao kushiriki mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa kupata elimu sahihi ya kimazingira ili kupata weledi na stadi muhimu zitakazowezesha kumudu kujitengenezea kipato kwa kuajiriwa na kujiajiri.

"Moja ya vikwazo vikubwa kwa vijana ambao utafiti unaonesha kutokuwa na kipato ni miongoni mwa yanayosababisha vijana walio wengi kutumbukia katika matumizi ya dawa za kulevya," alisema.

Aliongeza kuwa vijana wengi wamekuwa wanashawishika kwa fedha au ahadi kuwa kwa kujiingiza katika biashara hiyo na utumiaji dawa za kulevya, itakuwa rahisi kwao kuondokana katika umaskini, mtego ambao umekuwa ukiwanasa baadhi yao.

# Watiwa mbaroni tuhuma kuua na kuwachoma moto wasichana

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma limekamata watuhumiwa wawili wa mauaji ya wasichana wawili kwa kuwapiga na kuchoma moto katika chumba walimokuwa wanaishi na kuwasababishia kifo.

Tukio hilo lilitokea mapema wiki hii jiji hapa eneo la Nzuguni ambako wasichana hao walikuwa wakiishi.

Kamanda wa Polis mkoani Dodoma, Theopista Mallya alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo cha mauaji ya wasichana hao wawili. Alisema hakuna rukhsa yoyote ya raia kujichukulia sheria mkononi hata kama mtu amekukosea, bali kinachotakowa ni kuhakikisha anafikisha hoja husika kwa vyombo vya usalama ili ifanyiwe kazi.

"Ninawaonya watu msijichukulie sheria mkononi, mnapaswa kutoa taarifa kwa polisi, ndio wanajua cha kufanya na si vinginevyo," alisema Kamanda Mallya.

Kamanda Mallya alisema kuwa baada ya uchunguzi walikamata vijana hao ambao ni mafundi ujenzi waliotoa maelezo ya awali kuhusu tukio hilo.

Alisema wanaendelea na uchunguzi ili kubaini tukio zima mpaka kupelekea vifo vya wasichana hao wawili katika eneo la Nzuguni, jijini.

Kamanda huyo alitaka jamii kutoa taarifa pale inapoona kuna uhalifu unafanyika mahali popote na si kusubiri mpaka mauaji yatokee.

Alisema wasichana hao wamepoteza maisha bila sababu yoyote; majirani walipaswa kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ili kukamata watuhumiwa wa tukio hilo.

Katika hatua nyingine, kamanda huyo alisema jeshi hilo linaendelea na doria kwa ajili ya kuhakikisha maeneo yote yanakuwa salama.

Alisema doria zinafanywa kila mtaa, hivyo jamii inapaswa kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi ili kuhakikisha wahalifu wote wanakamatwa.



Mkuu wa mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi, akizungumza na wananchi na wachimbaji wadogo wa madini wa mgodi wa Kinyambwiga, Kata ya Guta, Halmashauri ya Mji wa Bunda juzi na kuwaagiza kuanzisha vikundi vya uzalishaji mali, ili iwe rahisi kwa serikali kuwatambua. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri afunga mgodi kisa vurugu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Antony Mavunde amesimamisha shughuli za uchimbaji madini katika mgodi wa dhahabu ulioko Kata ya Handali, wilayani Chamwino, mkoani Dodoma baada ya kuzuka vurugu baina ya wachimbaji wadogo na anayedaiwa kuwa mwekezaji kutoka China.

Vurugu hizo zilizuka juzi baada ya mtu huyo anayedaiwa kuwa mwekezaji kuingiza mtambo katika eneo hilo kwa ajili ya maandalizi ya uchimbaji ndipo wananchi walipojitokeza kuzuia.

Wakati wa vurugu hizo, inadaiwa kuwa mwekezaji huyo alimpiga ngumi mmoja wa wananchi hao waliokuwa wanazuia mitambo hiyo kufanya kazi katika eneo la machimbo.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Dodoma pamoja na Waziri wa Madini, Antony, walifunga safari hadi katika machimbo hayo na kuzungumza na wachimbaji wadogo na mwekezaji.

Akiwa katika machimbo hayo, waziri huyo aliagiza kufungwa mgodi huo hadi hapo mgogoro huo utakapotatuliwa na kupata suluhu ya kudumu ili jambo kama hilo lisitokee tena.

"Hikii kilichotokea hapa hakipaswi kujitokeza tena kama leo watu hadi wanapigana ngumi kwa sababu ya madini. Kama jambo hili likiachwa linaweza kuwa kubwa na wakati mwingine yakatokea maafa zaidi," alisema.

Waziri huyo alisema kuwa kutokana na eneo hilo kuwa na leseni ndogo ya uchimbaji madini ya PML ambayo ni kwa ajili ya wachimbaji wazawa, hapaswi kuingia mtu yeyote ambaye siyo Mtanzania.

"Leseni ndogo za PML ni kwa ajili ya wachimbaji wazawa pekee yake, hivyo ninaagiza hapaswi kuwapo mchimbaji mgeni ambaye siyo Mtanzania katika eneo hili tena.

"Katika maeneo haya asingie mgeni yeyote mpaka kuwe na msaada wa kiufundi, hivi sasa hapaswi kuwapo mgeni yeyote, niwaagize maofisa madini wa mikoa (RMO) kusimamia kifungu cha nane ya Sheria ya Madini, leseni ndogo hakuna mchimbaji wa nje kutumia," aliagiza huku akishangiliwa na wachimbaji hao.

Alisema wageni hawapaswi kwenda moja kwa moja katika mashimo ya uchimbaji madini badala yake wabaki kwenye masoko ya madini.

"Watu wanavunja kifungu cha nane na kuingia moja kwa moja katika mashimo, wageni wote kwa mujibu wa kifungu cha nane hawatakiwi kwenda katika mashimo ya uchimbaji madini, bali wabaki kwenye masoko ya madini," alionya.

Waziri huyo alisema kuwa kutokana na migogoro mingi katika mashimo hayo, mwezi huu zinaanza kutumika kanuni mpya ambapo atakayepewa leseni ya uchimbaji hatakiwi kuingiza wachimbaji wadogo.

"Mtu yeyote atakayepewa leseni ya uchimbaji asiingize wachimbaji wadogo, tunataka kuwaondoa madalali wa uchimbaji. Kuna wengine wababaishaji wanapewa leseni wanapangisha watu wengine," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliagiza Jeshi la Polisi kufuatilia suala hilo na kumhoji mwekezaji huyo anayedaiwa kumpiga ngumi mwananchi na hatua za kisheria zichukuliwe.





# Serikali yaweka mkakati kuongeza nyumba Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Nyumba Zanzibar leo linatarajiwa kuzindua nembo mpya ya shirika hilo ili kuleta mabadiliko ya kiutendaji katika shirika na kwenda sanjari na azma ya serikali ya kuongeza nyumba za makaazi zenye ubora kutokana na kuongezeka idadi ya watu na uhaba wa ardhi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Sultan Said Suleiman, alisema uboreshaji wa nembo umesababisha kuongezeka kwa imani ya wateja wa shirika hilo, wadau na wananchi kwamba shirika limejipanga katika kuleta kasi ya mabadiliko ya sekta ya biashara ya nyumba Zanzibar.

Alisema mwonekano huo mpya wa nembo ya shirika hilo utaakisi kasi ya soko la biashara kwa shirika katika ukuaji endelevu na utoaji huduma bora zinazoendena na mabadiliko katika sekta ya makaazi.

"Nembo mpya ya shirika inashabihiana na mahitaji ya sasa katika sekta ya majengo kwani inaweza kuonesha nyumba za ghorofa ambazo ndiyo zinazokwenda na wakati na ndiyo muelekeo wa serikali ya Zanzibar"alisema.

Alisema utambulisho wa nembo hiyo utasababisha shirika la nyumba kulitangaza na kuonekana na muonekano mpya katika sekta ya nyumba na makaazi Zanzibar.

Akizungumzia miradi ya shirika hilo ambayo wanatarajia kuitekeleza katika mwaka wa fedha wa 2024/2025, alisema shirika inakuja na mradi mkubwa wa nyumba bora na bei nafuu katika kijiji cha Kisakasaka visiwani humo.

Alisema mradi huo unahuduma zote muhimu na utakuwa na nyumba nyingi za makaazi na za kisasa, pamoja na mradi wa nyumba za biashara huko Nyamanzi visiwani humo.

Uzinduzi wa nembo hiyo mpya utafanyika katika viwanja vya biashara nyamanzi na Waziri wa Ardhi na Makaazi, Rahma Kassim Ali, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo.

# Samia aagiza waganga tiba asili kufuata maadili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka waganga wanaotoa matibabu ya tiba asili kufuata maadili na nidhamu kama inavyoelekezwa kwenye vitabu vya dini.

Aliyasema hayo jana katika kongamano la wanawake la mwaka mpya wa kiislamu wa 1446 visiwani Zanzibar lililoandalia na Ofisi ya Mufti wa Zanzibar.

Alisema serikali haina shida na tiba asili kwasababu inawasaidia watu wengi lakini kuna shida kwa baadhi ya wanaotoa tiba hiyo ambao wanajihusisha kupiga ramli chonganishi na kusababisha mtafaruku katika jamii.

"Kupiga ramli chonganishi ni moja ya sehemu ya imani potofu, dhulma na inatakiwa kukemewa kwa nguvu hivyo ofisi ya Mufti iendelee kutoa elimu na kujenga imani za watu ili wasishawishiwe na wapiga ramli,"alisema Rais Samia.

Aidha, alisema serikali itaendelea kufuatilia kuwabaini na kuwachukulia hatua waganga wanaopiga ramli chonganishi na kusababisha wakati mwingine watu kuuana.

Aliwashangaa viongozi wa kisiasa wanaowakashifu na kuwadhalilisha viongozi wanapokuwa majukwaani akisema kuwa anayepata malezi ya kimani hawezi kuwa na kasumba hiyo.

Alisema watu wanaopata mafunzo ya dini hawawezi kumkashifu au kumtukana kiongozi na kuongeza kuwa anaamini wanaofanya hivyo hawajapita katika mafunzo ya imani za dini.

Rais Samia aliwataka viongozi wa dini kuongeza jitihada ya kutoa elimu kwa vijana ili kuwa na lugha nzuri na kuwa watiifu na kuwaheshimu viongozi wao.

Pia, Rais Samia alisema viongozi nao wanawajibu wa kuendelea kuishi katika misingi ya uongozi bora kwa kuwa waadilifu na kuwasikiliza na kutatua shida za wananchi wanapokwenda kwao.

Akizungumzia suala la kodi, Rais Samia alisema hakuna serikali inayoendeshwa bila ya kodi hivyo wananchi wanapaswa kulipa kodi kwa hiyari kwa kuwa kodi imehimizwa hadi katika vitabu vya dini.

Alisema katika historia ya uislamu mwanamke ametukuzwa na kupewa nafasi ya juu lakini katika utekelezaji mambo hayendi sawa na wanaume.

Aliwataka viongozi wa dini kuacha kuwasimanga wanawake pekee wakati wa mahubiri yao na badala yake wawe wanawakemea baadhi ya wanaume ambao hufanya mambo ya ovyo kwenye jamii.

Rais Samia aliwataka wananchi kuendelea kuishi kwa amani na utulivu ili kuithamini tunu hiyo ya amani kwa kufanya ibada kwa utulivu na ili nchi ipate maendeleo kwani pasipo na amani hakuna maendeleo yatakayopatikana.

Katika kongamano hilo la wanawake katika kuupokea mwaka mpya wa kiislamu, mada mbalimbali ziliwasilishwa ikiwemo masuala ya kodi, kuwatii na kuwaheshimu viongozi.

Kongamano hilo limehuduhriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, viongozi wa dini na viongozi wa kisiasa.



Sehemu ya washiriki wa Kongamano la Wanawake wa Kiislam Zanzibar, wakifuatilia mada mbalimbali zilizokuwa zikitolewa katika kongamano hilo, jana. **PICHA: IKULU**

# Makandarasi watakiwa kuzingatia mikataba

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amewataka makandarasi wanaopewa kazi ya kujenga miradi Zanzibar kuheshimu mikataba wanayoingia na Serikali.

Aliyasema hayo jana wakati alipofanya ziara kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi Kuu ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Maisara, Wilaya ya Mjini Unguja.

Hemed alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya makandarasi kuchelewesha kumaliza kwa wakati miradi wanayopewa kujenga na kuomba kuongezewa muda jambo ambalo linakwamisha azma ya Serikali ya kutatua kero za wananchi kwa wakati.

Alisema Serikali ya Zanzibar itaendelea kuheshimu mikataba inayoingia na kampuni mbalimbali pamoja na kutoa ushirikiano wa hali kwa kampuni zinazojenga miradi ili kuharakisha ukamilishaji wa miradi hio kwa utaratibu uliopangwa na viwango vyenye ubora.

Alisema kumalizika kwa wakati kwa ujenzi wa jengo hilo kutatoa fursa kwa ZEC kufanya kazi zake katika mazingira mazuri na salama. Aidha, alisema kuanzia sasa Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) wanapaswa kuzichukulia hatua kali Kampuni ambazo hazitakabidhi miradi kwa wakati uliopangwa ili iwe fundisho kwa kampuni zingine.

Aliwataka wakala wa majengo kuacha kuzichekea kampuni zitakazo kwenda kinyume na mkataba wa ujenzi wa miradi ya Serikali ambayo wamesaini.

Naye mkandarasi kutoka kampuni ya China Railway Jianhuwang Engineering (CRJE), Chey Yur, alisema watahakikisha wanakamilisha na kukabidhi jengo hilo ndani ya muda waliokubaliana. Mkandarasi Yur alisema wameshaongeza nguvu kazi katika ujenzi huo na wanatarajia kuanza kufanya kazi usiku na mchana ili kuongeza kasi ya ujenzi na kukamilisha kwa wakati uliopangwa na kwa ubora zaidi.

Msimamizi wa majengo kutoka (ZBA), Mohamed Nahoda Mohamed, alisema ZBA imekuwa ikishirikiana kwa karibu na Mkandarasi wa ujenzi huo ambao kwa sasa umefikia asilimia 20 na wanatarajia kukamilisha mwishoni mwa mwezi Disemba mwaka huu.

Ujenzi huo wa Jengo la orofa nne la ZEC utakapokamilika utagharimu zaidi ya shilingi Bilioni 11 ambao utajumuisha Ofisi, Kumbi za Mikutano na vyumba kwa ajili ya wageni.



**JAY MELODY**

UKURASA 12

Nipashe
BT BURUDANI TELE
JUMAMOSI JULAI 6, 2024



# YAJAYO YANAFURAHISHA

WAKATI waigizaji wa Bongo Muvi wapo nchini Korea wakitafuta fursa, mambo yamekuwa ya moto baada ya watu wanaofuatilia ziara hiyo kuhisi kutaibuka mambo mazito.

Kitu cha kipekee kinachozungumzwa na wengi kwa sasa ni jinsi kuwapo kwa dalili ya kurudi upya kwa penzi kati ya wasanii maarufu nchini, Wema Sepetu na Idris Sultan.

Watu waliobahatika kuona baadhi ya video zinazoangazia ziara hiyo, wameeleza huenda waigizaji hao wakarudiana baada ya kumaliza ziara hiyo.

Moja ya video inayosambaa ni ile inayomwonyesha Wema akimuangalia Sultan kwa macho ya kimahaba, wakati wakitambulishwa kwa wenyeji wao.

Wawili hao ambao walikuwa wapenzi miaka ya nyuma na kisha kuachana, imeelezwa kwenye ziara hiyo wameonekana kutazamana kwa macho yaliyojaa upendo.

Hamisi Juma ambaye amekuwa akifuatilia ziara hiyo, amesema ziara hiyo inaweza kuwarudisha tena kwenye uhusiano, lakini sio kama wanavyohitaji mashabiki bali wao wenyewe.

"Wema anajulikana kuwa na macho ya kuvutia, kitendo cha kumtazama Sultan kwa macho ya kimahaba haitoi uthibitisho kwamba wamerudiana, ni suala la kusubiri," amesema Juma.

Amesema wasanii hao wanatambua kuwa kwenda kwao Korea Kusini ni jambo la maana kubwa, hivyo hawawezi kutumia fursa hiyo kufikiria mapenzi badala ya fursa ya kupata upeo mpana kuhusu tasnia hiyo.

BASI SAWA

## Loui asema yasiyosemwa



MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Loui, amesema ukimya wa wanamuziki wengi unatokana na ugumu wa kukabiliana na changamoto ya soko.

Amesema, kama msanii anahitaji kutoka haraka lazima awe na nguvu ya kutosha kutangaza kazi zake, vinginevyo anaweza kukaa ndani na nyimbo zake akizisikiliza na familia.

"Mimi sikukaa kimya kama wengi wanavyodhani, nilikuwa natoa kazi lakini kwa muziki wa sasa kama hujawa na fedha ya kutangaza unaweza kukaa nyumbani na ukageuza nyimbo maandazi ya kula," amesema Loui

## Sultan ashangaa Korea



MWIGIZAJI anayefanya vizuri katika soko la kimataifa, Idris Sultan, amesema anashangazwa na kitendo cha raia wa Korea Kusini, kufahamu kazi zake tofauti na alivyofikiria.

Sultan ambaye ni miongoni mwa wasanii wa Tanzania wanaofanya ziara nchini humo kujifunza kazi ya filamu, amesema jambo hilo limempa faraja na kumpa nguvu ya kufanya kazi kwa bidii.

"Sikutegemea kukutana na wakorea ambao wameona movie zangu. Ziara ya wiki moja tu Korea na kuna hasira nyingi sana za kazi zimenijaa," ameandika kupitia ukurasa wake wa Instagram.



## JAY MELODY KUMBE YALIMKUTA

MWANAMUZIKI wa Bongo fleva, Jay Melody, ameweka wazi kuhusu albamu yake mpya kukosa kolabo na wasanii wakubwa, akisema baadhi walimpa masharti magumu ambayo hayatekelezeki.

Amesema wakati akiandaa albamu hiyo 'Therapy' aliwalenga wasanii sita kufanya nao kazi, lakini alipowafuata walimpatia masharti ambayo ni vigumu kuyafuata.

"Nilikuwa nahofu mwanzo kuhusu kazi zangu, lakini nashukuru Watanzania wameipokea kwa furaha jambo ambalo hata mimi limenishangaza. Nilidhani itakuwa ngumu hasa katika kuitangaza," amesema Jay Melody.



## Acheni kumwandama Shakib

KUFUATIA madai ya kuwa anaishi kwa kutumia mgongo wa mkewe, Shakib Cham Lutaaya, ambaye ni mume wa Zari Hassan, amesema kamwe hawezi kuwa tegemezi na hata magari anayotembea nayo ni mali yake.

Shakib amesema yeye ana ukwasi wa kifedha kwani hata gari lake la kwanza kumiliki 2015, lilikuwa la gharama aina ya BMW.

"Watu wanasema eti nilikuwa naazima gari, mtu unaweza azima gari na ukae nalo kwa miaka 10? Niambie mtu mmoja ambaye amewahi fanya hivyo. Acha nikuambie, mimi nilimiliki gari aina ya BMW. Hilo lilikuwa gari langu la kwanza mwaka 2015. Sijui kwa pesa za Uganda ni shilingi ngapi lakini kwa Afrika Kusini ilikuwa Rand 20k," amesema Shakib.

## KIBOKO YA MANINJA

Na Adam Fungamwango

KWENYE miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000, Wabongo walikuwa hawashikiki kwa 'muvi' mbalimbali, zikiwemo za kizungu, kihindi, kijapani na kichina.

Kuna waliopenda filamu za kihindi walipenda zote za mapigano na mapenzi, lakini kwa hizo zilizobaki walipenda za kimapigano na kibabe.

Moja ya aina ya mapigano yaliyokuwa yameshangaza na kupendwa na wengi ni ya kininja.


Filamu za kininja zilijizolea mashabiki wengi miaka hiyo kutokana na staili yake ya wapiganaji wake ambao walionekana kama si watu wa kawaida, kwani walikuwa wepesi wa kila kitu, kuruka, kupanda juu, na hata wakati mwingine kupotea kimiujiza.

Walikuwa na uwezo wa kupigana kwa mikono na zana mbalimbali za kijadi. Huwa hawatumii bastola tu. Asili ya staili hii ni nchini Japan.

Pamoja hayo kulikuwa na 'mastelingi' ambao walikuwa ni kiboko yao. Yaani hao kwenye filamu hizo walikuwa wakiwashinda maninja na hila zao zote.

Hawa ni baadhi ya mastaa wa filamu ambao walikuwa ni kiboko ya Maninja.

### Michael Dudikoff




Huyu ni 'stelingi' Mmarekani ambaye alitamba sana miaka ya 1980 na filamu zake kali za maninja, na hasa alipotoa kwa mara ya kwanza picha ya ya kwanza American Ninja mwaka 1985.

Filamu hiyo ilifuatia tena na mfululizo za American Ninja namba mbili na kuendelea na kumpatia umaarufu mkubwa sana.

Kwa watazamaji wa picha wa wakati huo Bongo, wanamtazama staa huyu kuwa ni mmoja wa waliokuwa kiboko wa maninja, kwani pamoja na hila zao zote, lakini alikuwa akiwafyeka.

Kwenye picha alikuwa akicheza kama Mmarekani aliyepata mafunzo ya kininja na babu mmoja wa kijapani akiwa mdogo, na baadaye kuja kuwatesa 'Wajepu' wenyewe na 'Wavete' yaani Wavietnam.

### Alexander Low

Huyu ni bingwa wa zamani wa sanaa za mapigano staili ya 'taekwando' wa Taiwan. Huyu naye ni mtaalamu wa kuwaduwaza maninja. Ni kiboko wa maninja. Amecheza picha mbalimbali kama vile The Ninja Hunter, The Super Ninja, Ninja vs Shaolin na nyingine nyingi.

Kama alivyo Mmarekani Dudikoff, huyu naye alikuwa kipenzi cha mashabiki wengi wa filamu wakati huo, kutokana na uhodari wake wa kuwatwanga maninja ambayo wanachukuliwa ni watu katili na wakorofi kwenye 'muvi'.

### Sho Kosugi

Huyu sasa ni ninja halisi. Wakati hawa wengine wakicheza kama filamu tu, lakini Sho Kosugi ni ninja hasa na Mjapani, kule kule kulikotoka mchezo huo. Anacheza michezo yote ya sanaa za mapigano, kama katare, kendo, judo, laido, kobudo, aikido na ninjutsu ambao ndiyo staili wanayojifunza zaidi maninja. Jamaa ni bingwa wa zamani wa karate nchini kwao.

Kwa sasa anatengeneza filamu na kufundisha, lakini naye alikuwa ni mtaalam wa kuwagonga maninja kwenye filamu zake nyingi alizocheza na Wabongo wanamfahamu zaidi kwa jina la 'Shokoshugi'.

### Franco Nero

Ni mastaa wa mwanzo kabisa kucheza filamu za kininja. Jamaa ni Mtaliano, lakini alicheza filamu chache za kininja, ikiwemo Enter the Ninja, iliyotoka mwaka 1981. Ni mmoja wa mastaa ambao hawaimbwi sana kama wenzake hapa Bongo, lakini wale wenye kufutilia sana filamu za mapigano wanamfahamu sana na kumkubali mbabe huyu.

### Jet Li

Wala sina haja ya kumuelezea sana mbabe huyu kwani hata watoto wadogo leo hii wanamfahamu.

Staa huyu, mbali na kucheza filamu nyingi, lakini pia hakuacha baadhi ya filamu zake kupambana na maninja.

FILAMU

## Mfufumo: Mfalme wa mchongo

Na Adam Fungamwango

CHEO hakilazimishwi, bali huja chenyewe jinsi watu wanavyokukubali na kukuona unafaa kuwaongoza. Tumeona baadhi ya watu wanatumia pesa ili wapate uongozi, lakini wapo waliokubalika bila pesa wakashinda uongozi.

Leo tutaiangalia filamu iitwayo 'Mfufumo' tuone jinsi baadhi ya watu ambao wanalazimisha uongozi kwa njia yoyote ile, mradi tu wapate.

Imechezwa na wasanii Juma Mbega, Francis Malela, Elizabeth Singu, Happyness Masongo, Yohana Joseph na wengine wengi.

Inaanza kwa kuonyesha, mfalme wa himaya ya Mfufumo alitaka kumuandaa kijana wake kuwa mrithi wake, kwani umri wake unazidi kuwa mkubwa sasa.

Melela ndiyo anaandaliwa kuwa mfalme, naye anaitwa na baba yake kuambiwa atafute mchumba kwanza aoe. Kijana huyo anamtafuta msichana mmoja mrembo aitwaye Nchama ili awe mkewe kabla ya kurithi kiti cha baba yake.

Siku ya harusi, bibi harusi akapotea. Himaya nzima ikawa na taharuki. Kumbe bibi harusi alichukuliwa kimiujiza porini. Huko anakutana na mpenzi wake wa zamani Bilal, kwanza anamuogopa kwa sababu anajua ameshafariki. Bilal anamwambia ni kweli amefariki, lakini mzimu wake bado uko hai. Anamwambia kuwa kifo chake hakikuwa cha bahati mbaya, bali kilipangwa na mfalme wa sasa ili kijana wake Malela arithi kiti cha ufalme.

Mzimu wa Bilal ukamwambia mpenzi wake Nchama kuwa yeye ndiye aliyekuwa mrithi halali, kwani mfalme wa sasa ambaye ni baba yake mkubwa, alikuwa ameushikilia kwa muda baada ya baba yake mzazi kufariki. Na kwa sasa imefika zamu ya kulipiza kisasi. Bilal anamchukua Nchama na kwenda naye hadi kwenye harusi ambako walikuwa wanamtafuta.

Radi kubwa ikapiga, watu wote wakatawanyika. Ikawa ni hofu kubwa kijijini. Mfalme akaanza kuugua ugonjwa usiojulikana.

Mfalme ilibidi awaite wazee na kuwaeleza ukweli kuwa, alimuua mdogo wake ambaye alikuwa mfalme na kwa sababu mtoto wake Bilal alikuwa mdogo ilibidi arithi yeye kaka mtu hadi Bilal atakapokuwa mkubwa. Lakini hata alipokuwa mkubwa, akamuua na Bilal ili mtoto wake Malela ndiyo awe mrithi. Baada ya kueleza ukweli wote, 'mfalme wa mchongo' akafariki dunia.





# Falz watu hawatakuelewa

RAPA maarufu wa Nigeria, Falz amekiri kuwa hajawahi kuwa na uhusiano wa kimapenzi tangu akiwa na umri wa miaka 18, mwaka 2008.

Falz alifichua hayo kwenye kipindi cha Morning Rush Show, kinachoendeshwa na Bibi Rai, ambapo aliulizwa lini mara ya mwisho kushiriki mapenzi.

"Uhusiano wangu wa mwisho ulikuwa 2008; nilikuwa na umri wa miaka 18 kwa usahihi. Sio kama ninakimbia, naendelea kubadilika, na sijihisi kuwa tayari." Amesema Falz



## Simi ulijua dunia duara?

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Simi amesema kiingereza cha mitaani maarufu kama 'Pidgin' kilimpa wakati mgumu alipokwenda nchini Kenya.

Simi amesema awali alikuwa na mawazo tofauti kuhusu lugha hiyo, lakini baada ya tukio hilo amegundua Kiingereza hicho hakizungumzwi na Waafrika wote.

"Nilienda Kenya miaka ya nyuma, na tulitakiwa kufanya remix ya wimbo wangu na msanii wa Kenya, ndani kuna Pidgin nyingi, yule msanii aliniuliza ile ni lugha gani, nikamjibu ni Kiingereza na hapo nikagundua si kila mtu anazungumza," amesema

## Foolio aliuawa hivi....

POLISI wametoa video mpya inayoonyesha jinsi mwanamuziki wa Hip Hop wa Marekani, Julio Foolio, alivyouawa kwa kupigwa risasi,

Video hiyo inamuonyesha mtu mwenye silaha akilimiminia risasi gari la msanii huyo nje ya hoteli

Foolio alikuwa katika jiji hilo akisherehekea na marafiki zake na baadae walielekea katika hoteli hiyo kwa nia ya kuendelea kula bata, kabla ya kupigwa risasi wakati akiwasili eneo hilo na gari lake la rangi nyeusi.





## Davido afichua Fungate yake

MKALI wa muziki wa Afrobeat, Davido, ametoa kwa mara ya kwanza video inayoonyesha sehemu alipokwenda fungate na mkewe Chioma, baada ya kufunga ndoa.

Davido aliwafurahisha mashabiki zake baada ya kufichua kuwa yeye, mkewe na watoto wao mapacha walikwenda Atlanta nchini Marekani kufurahia ndoa yao.


Mwanamuziki huyo alifunga ndoa na mpenzi wake huyo wiki iliyopita katika sherehe ya kifahari iliyovunja rekodi nchini Nigeria.

## Kanye tabu iko palepale

RAPA maarufu wa Marekani, Kanye West, ameingia katika mgogoro mwingine wa kisheria baada ya kuhusishwa na madai ya manyanyaso kwa wafanyakazi wake.

Inadaiwa Kanye aliweka mazingira ya kazi kuwa ya uadui, kutolipa wafanyakazi wa kampuni yake ya YZY, na kuwatumia picha na video za utupu.

Madai hayo yametolewa na mkuu wa wafanyakazi wake wa zamani, Milo Yiannopoulos, ambapo alidai kadhia hizo zilianza Aprili 2024 wakati Kanye alipojitayarisha kuzindua kampuni yake ya kuonyesha maudhui ya watu wazima, YZY Porn, na huduma ya kutiririsha muziki, YZYVSN.



# Kituo cha utafiti wa mboga kuwezeshwa Euro 600,000

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

KITUO cha Kimataifa cha Utafiti wa Mboga na Uhifadhi wa Mbegu (World Veg) kilichoko Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha kinatarajia kupokea Euro 600,000 kutoka Shirika la Chakula Duniani (FAO) kwa ajili ya kuwezesha Benki ya Mbegu (Gen Bank) kufikia malengo yake.

Jana Mkurugenzi Mkuu wa World Vegetable Center Ukanda wa Afrika, Dk. Gabriel Rugalema, alisema wanatarajia fedha hizo zitawasaidia katika shughuli ya kuhifadhi mbegu za asili ambapo kwa sasa wanaendelea kuweka vinasaba katika benki hiyo.

Alikuwa akitoa taarifa kuhusu mpango wa kupatiwa fedha hizo kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo.

Kuhusu Benki ya Kuhifadhi Mbegu (Gen Bank), Dk. Rugalema alisema: "Tumeshafikia wakulima 504, wanafunzi 120 na watu wa nje zaidi ya 600, wamepata elimu ya masuala ya kilimo cha mboga, hivyo kituo hiki kina umuhimu mkubwa kwenye kuleta ustawi wa kilimo nchini."

Katika hatua nyingine, kiongozi huyp alisema ulaji mboga bado ni mdogo kwa jamii ingawa zina umuhimu mkubwa kwenye mwili wa binadamu ikiwamo kuimarisha afya na kupambana na magonjwa.

"Shirika la Afya Duniani (WHO) linapendekeza mtu kula angalau gramu 50 za mboga kwa siku, ili kufikisha kilogramu 80 kwa mwaka, hivyo hamasa inatakiwa kutolewa kuhusu umuhimu wa mboga kwenye lishe," alisema Rugemalila.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Bunge, Mariam Mzuzuri alisema kuwa kutokana na kazi nzuri inayofanywa na kituo hicho, watapeleka mapendekezo yao kwa wizara husika ili yafanyiwe kazi.

"Kituo kimekuwa na eneo dogo na tumeambiwa walishatuma maombi ya kuongezwa eneo ili kujipanua na wafanye kazi zao kwa ufanisi, hilo tumelibeba na tutahakikisha linafanyiwa kazi kwa haraka," alisema Mariam.

Mjumbe wa Kamati hiyo na Mbunge wa Babati Mjini, Pauline Gekul, alisema kulingana na utafiti unaofanywa na kituo hicho, ni vyema ukafanyika utafiti wa udongo kwa kila mkoa na kutambua mboga gani inafanya vizuri eneo hilo na kuisogeza kwa wananchi.

# Wavuvi haramu wajisalimisha kwa RC kukwepa kushtakiwa

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAVUVI 10 kati ya 17 waliokuwa wanajishughulisha na uvuvi haramu wa kutumia mabomu Bahari ya Hindi, wamejisalimisha wakiwa na vifaa vyao kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dk. Batilda Buriani ili kukwepa mkono wa sheria.

Juni 6 mwaka huu, Mkuu wa Mkoa huyo aliposhiriki maadhimisho ya Siku ya Matumbawe, alitoa ilani, akitaka kwa hiyari yao wavuvi hao kujisalimisha wenyewe.

Aliagiza wavuvi wote wanaovua kinyume cha taratibu wajisalimishe wenyewe ofisini kwake kabla ya kuanza operesheni ya kuwatafuta kwa nguvu, kwa kuwa anayo majina yao na yuko tayari kushughulika nao kutokana na kuathiri uchumi wa bluu.

Baada ya kukabidhiwa vifaa hivyo, Mkuu wa Mkoa Dk. Batilda alisema kuwa baada ya kutafakari zaidi, aliona atoe ilani kabla ya kulitumia Jeshi la Polisi kukimbizana na wavuvi haramu.

"Ni ukweli usiofichika kwamba Mkoa wa Tanga una bahati ya kuwamo katika ukanda wa bahari, na kina takribani kilomita 130.

"Kwahiyo, wengi waliozaliwa maeneo hayo, bahari ndio mashamba yao; na sisi tukiwa viongozi tunaangalia jinsi gani ya kuwasaidia kulima humo katika njia inayostahili.

"Tukiendа ndivyo sivyo, tutapata leo lakini kesho tutakosa na pia hicho tutakachokipata kitakuwa hakina thamani kwa maana kitaleta madhara kiafya na pia tutakwenda kuua yale mazalia ya viumbe wengi ndani ya bahari (matumbawe)," alifafanua.

Mkuu wa Mkoa akizungumzia umuhimu wa matumbawe, alisema mbali na kuwa ni mazalia ya viumbe, pia yanazuia mmomonyoko wa ardhi ikiwa ni pamoja na maji ya chumvi kutoingia nchi kavu na yanasaidia kunyonya chumvi baharini. "Wengi wakiona matumbawe wanajua ni mawe tu ya baharini, lakini vile ni viumbe, yana manufaa makubwa, na ukiona sehemu miamba ya matumbawe imeshavunjwa ni lazima mmomonyoko wa ardhi utatokea. "Matumbawe yana mchango mkubwa, na zaidi kuna viumbe aina tofauti wapatao 800 mazalia yao yapo katika matumbawe.

Kwahiyo, mnapovua iwe kupiga mabomu, mnaua hadi mayai ya samaki na biashara yenu inakuwa siyo endelevu, lakini pia faida yake si kubwa.

"Hapa Tanga kwa sasa tuna wavuvi 15,000, wadogo na wakubwa na wengi ndio wamo katika uvuvi huu haramu," alionya.

Mwarabu Mustapha, maarufu Gebo, Mkazi wa Mwarongo, Kata ya Tongoni, jijini Tanga alisema, "Matatizo niliyopata mimi ni makubwa sana kiasi ambacho hata nikihadithia ninajiskia kulia, nusura nipoteze uhai wangu baada ya kukamatwa nikifanya uvuvi haramu. Sasa ninamwahidi Mkuu wa Mkoa kwamba sitakaa nirudie tena na vifaa vyangu ninamkabidhi hapa."

Mwenyekiti wa Kamati ya Hifadhi, Mtaa wa Mwarongo, Aboubakari Nundu alisema, "Baada ya maagizo ya mkuu, nilichukua uamuzi wa kwenda mtaani kwangu kwa hawa wenzangu ambao ni waathirika, ninashukuru walinipokea na tukaelewana baada ya kuwahamasisha."




Mtumishi wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), mwenye uoni hafifu, Khadija Salum (kulia), akionyesha kitabu cha nukta nundu kwa mmoja wa wananchi waliotembelea banda la TET, katika maonyesho ya 48 ya biashara ya kimataifa Dar es Salaam, katika uwanja wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa jana. Taasisi hiyo, imekuwa ikiendelea kuwaelimisha Watanzania kuhusu umuhimu na manufaa ya mtaala mpya wa elimu ulioboreshwa. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Mradi wenye hoja za CAG wahitaji huruma za Ofisi ya Rais - TAMISEMI

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WILAYA ya Hai, mkoani Kilimanjaro inasubiri huruma ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuipa Sh. milioni 65 kwa ajili ya umaliziaji mradi wa ujenzi wa miundombinu katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Machame.

Mradi huo una hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ambaye katika ukaguzi wake kwa mwaka 2022/23, alibaini utaongeza gharama kubwa kwa serikali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dionis Myinga, akieleza hatua zilizochukuliwa ili kuifunga hoja hiyo ya CAG, alisema wamelazimika kuiandikia barua Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili kupata fedha za ziada za kuwezesha kukamilika mradi huo.

Alikuwa akitoa ufafanuzi juzi katika kikao maalum cha Baraza la Madiwani lililoketi kujadili hoja za CAG kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30 mwaka 2023.

CAG alitoa mapendekezo sita kuhusu hoja ya kuchelewa kukamilika ujenzi wa miundombinu ya shule hiyo iliyopewa na serikali Sh. milioni 372.6.

"Menejimenti imefanya ufuatiliaji wa karibu na kuweka juhudi zaidi katika kusimamia mradi huo ili kuhakikisha shughuli zilizobaki zinakamilika bila kuchelewa na kupata thamani ya fedha, ambapo bweni moja, vyumba vinne vya madarasa na vyoo matundu sita vimekamilika," alieleza Myinga.

Mapendekezo ya CAG ni pamoja na kutaka kuharakisha utekelezaji shughuli za mradi ili kuepusha uwezekano wa kuongezeka gharama kwa jumla ya fedha zilizotolewa.

Kuongeza juhudi katika kusimamia miradi inayotekelezwa kwa lengo la kupata thamani ya fedha kwa miradi iliyo ndani ya halmashauri mara fedha zinapotolewa.

Pendekezo lingine ni kuanzishwa mawasiliano na mamlaka inayohusika ili kushughulikia uwezekano wa kuongeza fedha za ziada kwa ajili ya kukamilisha shughuli za miradi.

Limo pia pendekezo la kutaka kuhakikisha mambo yanayosababisha kuongezeka gharama yanazingatiwa na mamlaka wakati wa utoaji fedha kwa ajili ya miradi ya baadaye.

Vilevile, CAG amependekeza kuanzishwa njia za wazi za mawasiliano na mafundi jamii, ili kuhakikisha wanafahamishwa kuhusu hitaji la kuomba kuongezwa muda, iwapo kuna ucheleweshaji wa mradi na kutoa maoni ya kurefusha mara moja ili kuepusha usumbufu na migogoro isiyo ya lazima ya mradi.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Wimbo 'Mambo kwa Soksi' wa Remmy ulivyokataliwa kurekodiwa studio RTD

## -Leo hii angepewa tuzo kuhamasisha kutomeza gonjwa hatari la Ukimwi
## -Nyimbo zenye ukakasi wa maneno yasiyofaa siku hizi zimejaa tele

**Na Adam Fungamwango**

MIAKA ya hivi karibuni tumeshuhudia nyimbo nyingi hasa za muziki wa kizazi kipya zikiwa na maneno yenye ukakasi mkubwa sana. Nyimbo zimekuwa na maneno ambayo si mafumbo, wala nahau, badala yake yamekuwa ni maneno yanayotafsirika moja kwa moja hata kwa watoto wadogo.

Na mbaya zaidi si maneno mazuri kwenye jamii. Baadhi ya wasanii wa kizazi kipya wanaona kuwa kuimba maneno yenya utata ndiyo nyimbo itapendwa au kupokelewa vizuri na mashabiki. Na nadhani hata mashabiki wa muziki wa sasa baadhi yao wamekuwa ni mashabiki na maneno haya.

Zamani ili wimbo ukubalike kurekodiwa ni lazima uweke maneno ambayo hayatotafsirika moja kwa moja kwa jamii. Ni lazima wale wenye kutazama kwa jicho la tatu, washairi na malenga ndiyo wanaoweza kujua nini kinaimbwa na tafsiri yake ni nini.

Mfano kuna wimbo mmoja wa taarabu 'Bunduki bila risasi yaua namna gani', ulioimbwa na marehemu bi Shakira Said. Ni aghalabu sana kugundua nini alichokuwa akikikusudia, tofauti na baadhi ya wasanii wa sasa ambao wamekuwa wakiweka wazi sana.

Kuna baadhi ya nyimbo za bendi mbalimbali ambazo hadi leo hii hazijarekodiwa hadi bendi hizo zimekufa, zingine zilirekebishwa maneno wakati wa kurekodi na zingine zilipigwa marufuku baada ya kurekodiwa.

Redio Tanzania au RTD, wakati huo ambayo kwa sasa ni TBC, ilikuwa na kamati iliyokuwa inapitia maneno ya nyimbo zote ambazo zililetwa kurekodiwa. Ni kwamba kabla ya kurekodi, bendi zililazimika kuleta mashairi ya nyimbo zote na kamati inayapitia neno kwa neno. Huko ndiko baadhi ya maneno yanakatwa na kuambiwa watumie maneno ambayo kamati imependekeza au ambayo wanamuziki wenyewe wataona inafaa. Baada ya kurekebishwa bendi inakwenda kurekodi.

Na siyo hivyo tu, inawezekana wimbo ukarekodiwa, lakini baada ya kutoka wananchi wakaupokea vinginevyo tofauti na ilivyotarajiwa, basi inaweza pia ukazuiwa kupigwa redioni.

Lengo la kamati kuzipitia, kuzirekebisha, kuzikataa, na hata kuzipiga marufuku baadhi ya nyimbo ni kutoifanya jamii ya Watanzania kupotoka, kutoka kwenye utamaduni wao halisi na kuiga ya wengine, kuheshiana, kuwa na adabu na heshima, yaani mkubwa na mdogo kuheshina, kusimamia maadili ya Kitaifa, lakini pia kuwafanya kuwa wamoja, wenye amani, utulivu na mshikamano.

Zipo nyimbo zilizorekodiwa lakini zikapigwa marufuku baadaye, zilizorekebishwa maneno ambapo awali zilikuwa na maneno mengine.

Zilizokataliwa zikabaki kupigwa kwenye kumbi tu, za zilikuwa zinapendwa na mashabiki wengi.




'Mambo Kwa Soksi'. Ni wimbo uliopigwa na Super Matimila ya Dr Remmy Ongalla akiimba yeye mwenyewe na Cosmas Thobias Chidumule. Ulikuwa unahimiza utumiaji ya mipira ya kiume, hasa wakati ule miaka ya 1980, ndiyo kwanza Ukimwi ulikuwa unaingia nchini na wengi hawakuwa na elimu hiyo.

Kama ingekuwa sasa, Wizara ya Afya ingeweza kumpa tuzo, kwani aliwahimiza wanaume kutumia mipira hiyo, na akawatahadharisha madhara ya kutofanya hivyo kuwa ni kupata maambukizo ya VVU na baadaye kifo.

Tena ilikuwa kwenye kipindi ambacho hata vidonge vya kufubaza havikuwepo, au kama vilikuwapo basi ni watu wachache sana ambao wenye uwezo ndiyo walibahatika kuvipata. Hospitali zetu bado zilikuwa hazijaa kutoa bure.

Wagonjwa wa wakati huo walionekana wazi kunapoupata kutokana na kukumbwa na magonjwa nyemelezi ambayo yaliwafanya hata kutengwa na kunyanyapaliwa.

Kwa bahati mbaya sana bado nchi ilikuwa na usiri kuhusu mambo hayo, tofauti na sasa, ambapo ugonjwa huo na hata jinsi ya kujikinga unazungumziwa kwa uwazi mkubwa, kiasi kwamba kuna matangazo kwenye redio na televisheni, vipeperushi na hata mabango. Wimbo ukapigwa marufuku.

Remmy alikuwa mjanja tangu zamani, wimbo huo akaenda kuurekodi nchini Kenya, hivyo watu walikuwa na kanda zao mitaani wakiusikiliza, lakini huwezi kuusikia kwenye redio.

HABARI KIMATAIFA

# Labour yapata ushindi wa kihistoria Uingereza

**LONDON,** UINGEREZA

CHAMA cha Labour kimeshinda kwa kunyakua viti vingi katika uchaguzi mkuu wa Uingereza uliofanyika juzi.

Kulingana na matokeo, Chama cha Labour kinachoongozwa na Keir Starmer, kimejinyakulia viti 326, ambavyo vinatoa nafasi ya kuunda serikali mpya.

Baada ya ushindi huo, waziri mkuu mtarajiwa Starmer, alizungumza akiwa jijini London kuwa amesikia sauti ya Waingereza na mabadiliko yanaanza sasa.

"Nahisi vizuri, lazima niseme ukweli," aliuambia umati wa watu waliokuwa wakishangilia.

Hata hivyo, akizungumza muda mfupi, Waziri Mkuu anayeondoka Rishi Sunak alikubali kushindwa, na kuwaambia wanachama wenzake kuwa ulikuwa uamuzi wa kutisha.

Sunak alisema anakubali kuwajibika kwa kushindwa kwa chama cha Conservative katika uchaguzi huo mkuu.

Sunak aliwaambia wafuasi wake kuwa watu wa Uingereza wametoa uamuzi mzito usiku wa juzi na kuna mengi ya kujifunza.




Waziri Mkuu mtarajiwa wa Uingereza Keir Starmer

Mpaka jana jioni zaidi ya viti 500 kati ya 650 matokeo yake yalitangazwa na chama cha Labour kilipata ushindi mnono.

Conservative kimendikisha matokeo mabaya zaidi katika historia yao kwa kupoteza zaidi ya viti 170 na wanatabiriwa kubakia na wabunge 136 pekee.

Ushindi huo ulimfanya Starmer kuwaambia wafuasi wa chama chake kuwa nchi hiyo inaamka kwa mwanga wa jua wa matumaini ambayo yanaangazia kwa mara nyingine baada ya miaka 14.

STARMER ALIKOTOKA

Keir Starmer, alianza maisha yake ya kitaaluma kama wakili katika miaka ya 1990, na aliteuliwa kuwa mkurugenzi wa mashtaka ya umma, mwendesha mashtaka mkuu wa uhalifu nchini Uingereza na Wales, mwaka wa 2008.

Alichaguliwa kwa mara ya kwanza kuwa mbunge wa Holborn na St Pancras kaskazini mwa London mnamo 2015, alichukua uongozi wa Labour baada ya uchaguzi mkuu wa chama wa 2019.

Katika uchaguzi huo aliahidi kuanza awamu mpya baada ya uongozi wa mrengo wa kushoto wa Jeremy Corbyn.

Starmer, alichaguliwa tena ubunge wa eneo hilo juzi, akinadi sera ya mabadiliko na kuahidi kukomesha siasa za kuigiza.

"Mabadiliko yanaanza hapa hapa kwa sababu hii ni demokrasia yako, jamii yako, maisha yako ya baadaye," alisema katika hotuba yake ya kuwashukuru wapiga kura.

Aliongeza "Umepiga kura. Sasa ni wakati wa sisi kufanya kazi."

**BBC**



Watu waliokimbia mapigano katika mji wa Singa, mji mkuu wa jimbo la Sennar kusini-mashariki mwa Sudan, wakiwasili eneo la Gedaref kukimbia mapigano kati ya Jeshi la Serikali na kikosi cha RSF juzi. **PICHA: AFP**

# Rais Ruto atangaza kubana matumizi

**NAIROBI,** KENYA

RAIS William Ruto wa Kenya, ameteua kikosi kazi huru kwa ajili ya kuchunguza deni halisi la taifa hilo, katika jitihada ya kubana matumizi ya serikali.

Akihutubia taifa hilo jana akiwa Ikulu ya Nairobi, Rais Ruto, alisema kuwa deni la nchi hiyo linaendelea kuwa sehemu ya ushiriki na mazungumzo nchini humo.

"Leo nimeteua kikosi kazi huru cha kufanya ukaguzi wa kina juu ya deni la umma na kuripoti kwetu katika miezi mitatu ijayo," alisema Rais Ruto.

Kiongozi huyo alisema katika kupunguza matumizi idadi ya washauri serikalini itapunguzwa kwa asilimia 50.

"Idadi ya washauri katika serikali itapunguzwa kwa asilimia 50 ndani ya utumishi wa umma haraka," alisisitiza.

Alieleza bajeti zilizotengewa Ofisi ya Mke wa Rais na Naibu Mke wa Rais, na Mke wa Waziri Kiongozi zimeondolewa.

Alisema kwamba mpango wa kuwaajiri maofisa wakuu wa utawala umesitishwa na kutangaza kukatwa asilimia 50 ya bajeti ya ukarabati wa majengo ya serikali.

Kuhusu ziara za viongozi wa kiserikali na wabunge nje ya nchi, Rais Ruto ametangaza kuwa safari zisizo na muhimu za viongozi zimesitishwa.

Katika hotuba hiyo, kiongozi huyo alitangaza kuwa utoaji wa michango ya pesa za misaada kwa viongozi wa serikali al maarufu na michango ya harambee umesimamishwa na badala yake serikali itaweka mfumo wa utoaji wa misaada hiyo.

Aliongeza kwenye hotuba hiyo kuwa mabadiliko hayo yanalenga kuboresha huduma za serikali kwa umma na kuhakikisha wananchi wanapata huduma kamili wanazohitaji kutoka serikalini.

Aidha, Rais Ruto alitoa mwaliko wa mazungumzo ya moja kwa moja yaliyopewa jina la "Engage" kupitia mtandao wa X Space kati yake na vijana wanaojiita Gen Z, ambao wamekuwa wakiandamana kupinga nyongeza ya ushuru tangu Juni 18.

Maandamano hayo ambayo yamegeuka na kuwa maandamano ya kuipinga serikali kutokana na masuala ambayo hayajashughulikiwa, yamesababisha vifo vya zaidi ya watu 40, huku mamia wakijeruhiwa au kukamatwa.

**BBC**

# Rais Biden njia panda

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani, Joe Biden, ameendelea kukabiliwa na shinikizo kujitoa kwenye kinyang'anyiro cha urais kupitia chama cha Democratic, katika uchaguzi utakaofanyika Novemba mwaka huu.

Baadhi ya magavana na wabunge kutoka chama chake wanasubiri mahojiano atakayofanya Biden na kituo cha utangazaji cha ABC, kuamua ikiwa waendelee kumuunga mkono au kuongeza shinikizo la kumng'oa kuwa mgombea wa chama chao.

Shinikizo hilo linatokana na Biden kushindwa kwenye mdahalo wake na Dobald Trump wa chama cha Republican yaliyofanyika wiki iliyopita.

Makamu wake, Kamala Harris, anaangaliwa kuwa mtu pekee atakayewania urais, endapo Biden atalazimika kujitoa.

Hata hivyo, Ikulu ya White House ilisema kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 81 hana mpango wa kuchukua hatua hiyo.

**DW**

# Russia yatoa sharti jipya kwa Ukraine

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladmir Putin, amesema hawezi kutangaza kusitisha vita bila ya serikali ya Ukraine kukubali masharti ya nchi yake.

Kiongozi huyo alisema Ukraine inaweza kutumia nafasi ya usitishaji vita kujihami kwa mashambulizi mapya, hivyo inabidi kwanza kufanyike mazungumzo ya kupata suluhisho endelevu.

Rais Putin aliyasema juzi na aligusia makubaliano yaliyofikiwa huko nyuma kuhusu vita hivyo vya Ukraine ambayo yaliishia kutupwa na pande zote mbili.

Kauli ya Putin inakuja wakati viongozi wa Umoja wa Ulaya jana walizungumzia wasiwasi wao kuhusu tetesi kuhusu Waziri Mkuu wa Hungary, Viktor Orban anayeshikilia uenyekiti wa umoja huo kwa sasa, anajiandaa kwenda Russia.

Rais wa baraza la Umoja wa Ulaya, Charles Michel alisema Orban hana mamlaka ya kuchukua hatua hiyo.

Michel alisema Russia ni mchokozi na Ukraine ni muhanga kwa hivyo hakuna mazungumzo kuhusu yanayoweza kufanywa bila ya Ukraine kuwepo.

**DW**

# Trilioni 1.7/- zakopeshwa sekta ya kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

MIKOPO yenye thamani ya Sh. trilioni 1.7 imetolewa katika kipindi cha miaka mitano kuwezesha sekta ya kilimo kupiga hatua na kuongeza tija kwa wakulima wadogo, wa kati na wakubwa.

Kwenye Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (Sabasaba) jana, Meneja Mwandamizi wa Idara ya Kilimo-Biashara wa Benki ya NMB, Neema Melleyeck alisema mikopo hiyo imetolewa na benki yao katika kipindi tajwa.

Alisema siri ya mwamko wa wadau wa sekta ya kilimo kuchangamkia mikopo ya kilimo-biashara ni riba nafuu, elimu, ushauri na masuluhisho ya kifedha wanayotoa.

Meneja huyo alisema sekta ya kilimo inayotajwa kuchangia asilimia 30 ya Pato la Taifa na kuajiri zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania, ni mnyororo wa thamani unaojumuisha kilimo chenyewe, uvuvi na ufugaji, ambako benki yao inakopesha na kuwawezesha wadau wake kwa kushirikiana na taasisi washirika, ikiwamo kampuni ya Agricom Tanzania.

Alisema NMB kwa kutambua umuhimu wa sekta ya kilimo kwa uchumi wa Tanzania, ilishusha riba ya mikopo ya kilimo hadi kufikia tarakimu moja (asilimia tisa) pamoja na kutia saini makubaliano na Agricom kuhakikisha wakulima wanakopeshwa matrekta, zana nyingine za kilimo na pembejeo.

"Lengo kuu ni kuiwezesha sekta ya kilimo kupiga hatua nchini, lakini pia kuongeza tija kwa wakulima, wadogo, wa kati, wakubwa na wadau wote wa mnyororo huo wa thamani unaojumuisha pia wavuvi na wafugaji, ambao licha ya kukopeshwa, hupewa elimu na ushauri juu ya mikopo yao kwa ufanisi wao kiuchumi.

"Hii imetufanya NMB kuwa benki tunayoongoza kunufaisha wadau wa sekta hii, ambapo tayari tumeshatoa mikopo ya zaidi ya Sh. trilioni 1.7 ndani ya miaka mitano hadi mwaka jana, wanufaika wakiwa wakulima wa kada zote na wafanyabiashara ha zinazofungamana na kilimo.

"Mwamko mkubwa wa Watanzania kukopa umetokana na NMB kushusha riba hadi kufikia asilimia tisa, tukijielekeza zaidi katika mikopo ya Stakabadhi Ghalani, Kilimo cha Mkataba na Mikopo ya Uwekezaji kwenye kilimo na kuongeza uzalishaji mazao," alisema Neema.

Alifafanua kwamba mikopo ya benki katika sekta ya kilimo inaanzia pale mkulima anapochagua ardhi, anapolima, anapopanda mbegu, kupalilia, kuvuna, kupeleka sokoni na kuwaunganisha wakulima na wadau wengine wakiwamo wateja wa mazao yao.

"Mkulima anaweza kukopa zana za kilimo kwa kulipa asilimia 20, kisha benki inamdhamini asilimia 80 na jambo jema ni ukweli kwamba NMB si tu mikopo, bali elimu sahihi inayozunguka sekta yenyewe, riba nafuu na huduma zenye masuluhishi ya kifedha," alisisitiza.




Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA), Kitengo cha Bandari, Alfred Shungu (kulia) akitoa elimu ya vipimo kwa mdau aliyetembelea banda la WMA, katika maonyesho ya 48 ya biashara ya kimataifa Dar es Salaam, katika uwanja wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa juzi. Katikati ni Meneja Sehemu ya Upimaji, Robert Makule. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## WMA yanunua mitambo ya kisasa kuhakiki mita za umeme

**Na Joseph Mwendapole**

KATIKA jitihada za kwenda na mabadiliko ya teknolojia duniani kwenye masuala ya vipimo, Wakala wa Vipimo (WMA) umenunua mitambo mitatu ya kisasa ya uhakiki wa mita za umeme.

Hayo yalisemwa juzi kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam na Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa WMA, Paulus Oluochi, wakati akizungumza kwenye maonesho hayo.

Oluochi alisema mitambo miwili iko katika Kituo cha Uhakiki eneo la Misugusugu, Mkoa wa Pwani na mtambo mmoja uko mkoani Kilimanjaro.

Alisema kununuliwa mitambo hiyo kumeleta ufanisi mkubwa kwenye eneo la uhakiki wa mita za umeme na kwamba tayari wameshaanza kuhakiki mita hizo tangu mwezi Machi mwaka huu.

Alisema kuanzia mwezi Machi mwaka huu, mita zote zinazotoka nje ya nchi na zile zinazotengenezwa nchini zimekuwa zinahakikiwa na WMA ili kuhakikisha hazimpunji mteja wa mwisho.

"Uhakiki wa mita mpya za umeme ulianza mwezi Machi na zaidi ya mita 2,000 zimeshahakikiwa ikiwa ni utekelezaji Sheria ya Vipimo, Sura Na. 340 na mita zote kabla ya kufungwa kwa wateja zinakuja kwetu tunazipima na kama hazina shida zinafungwa kwa wateja," alisema Oluochi.

Alisema WMA inaendelea kusimamia usahihi wa vipimo katika sekta mbalimbali na inaendelea kuwajengea uwezo wa kitaalamu watumishi wake mara kwa mara ili kuzidi kuingia katika maeneo mapya ya utendaji kazi.

Alisema kwenye maonesho hayo, WMA imeendelea kutoa elimu ya usahihi wa vipimo na kuwataka wafanyabiashara waache tabia ya kufungasha bidhaa kwa mtindo wa lumbesa.

Alisema WMA imekuwa ikifanya operesheni za mara kwa mara kukagua kama wafanyabiashara wanazingatia vipimo sahihi na wale wanaokutwa wakikiuka hutozwa faini, wakiwamo wafanyabiashara wanaofungasha kwa mtindo wa lumbesa.

Ofisa huyo alisema kuwa katika maonesho hayo, WMA imejikita katika kutoa elimu ya matumizi sahihi ya vipimo katika maeneo mbalimbali ya biashara, afya, mazingira na usalama kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala mbalimbali ya vipimo.

Alisema lengo la WMA ni kuwajengea ufahamu wadau na wananchi kwa ujumla juu ya utendaji kazi wa WMA katika uhakiki wa mita za umeme, dira za maji na vipimo vingine mbalimbali.

Alisema katika namna ya kipekee, WMA pia inaendelea kutoa elimu kwa wadau na wananchi kwa ujumla juu ya ufungashaji sahihi wa mazao katika uzito wa kilogramu 100 kama Sheria ya Vipimo, Sura Na. 340 inavyoelekeza.

Alisema wamekuwa wakiwasisitiza wafanyabiashara wajiepushe kufungasha mazao ya shamba kwa uzito unaozidi kilo 100 maarufu kama lumbesa kwa kuwa kufungasha hivyo ni kosa kisheria.

"Tunaendelea kutoa elimu kwa wauzaji wa mazao mbalimbali kuuza kwa kutumia mizani sahihi iliyohakikiwa na si kwa kutumia makopo, visado na ndoo na wito unatolewa kwa wanunuzi wote wa bidhaa kutumia mizani katika ununuzi wao wote katika masoko na maduka ya kuuzia bidhaa," alisema.

Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba) yalifunguliwa rasmi Julai 3 mwaka huu na Rais wa Filipe Nyusi aliyeambatana na mwenyeji wake, Rais Samia Suluhu Hassan.

## Wastaafu wa TANESCO waomba kulipwa posho

**Na Elizabeth Zaya**

WASTAAFU wa Shirika la Umeme (TANESCO), wameomba serikali kuangalia namna ya kuwapatia posho kidogo ili iwasaidie kumudu changamoto mbalimbali za maisha ambazo wamekuwa wakikutana nazo baada ya utumishi wao.

Wamesema kuna tatizo kwa watumishi wengi wa umma kushindwa kumudu gharama za maisha baada ya kustaafu na hivyo kuishi maisha magumu ambayo wakati mwingine huchangia wengi wao kufariki dunia muda mfupi baada ya kustaafu.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wastaafu wa TANESCO, Boniface Njombe, amesema kuwa pamoja na pensheni ambayo wamekuwa wakipewa baada ya kustaafu, imekuwa haitoshelezi kumudu gharama za maisha zinazopanda kila kukicha.

"Tunafahamu kwamba kila baada ya muda fulani, serikali hupandisha mshahara kwa wafanyakazi ili waweze kumudu gharama za maisha mbalimbali, wakati wenzetu wanapandishiwa mishahara, kuwawezesha waishi vizuri, wastaafu bado pensheni yetu imebaki palepale na hakika tunapata shida sana kumudu maisha," alisema mmoja wa wastaafu wa TANESCO waliozungumza na Nipashe jijini Dar esv Salaam jana.

Aliongeza, "Huenda ndio sababu wastaafu wengi wanapata shida na wengine kufariki dunia mapema, kwa sababu ya matatizo kama hayo ya kushindwa kumudu maisha yao.

"Kwahiyo, tungeomba kwamba ikimpendeza Rais kupitia serikali yake, inapopandisha mshahara kwa ajili ya wafanyakazi, iangalie pia angalau kwa asilimia fulani wafanyakazi waliostaafu nao waongezwe kiwango kwa posho kwa kiasi fulani."

Wastaafu hao waliiomba serikali iendelee kuboresha matibabu kwa wastaafu hao kwa kuwawekea utaratibu wa bima ya afya.

"Katika umri wetu huu magonjwa nyemelezi ni mengi, upande wa matibabu pia wastaafu wengi, hasa tuliofanya kazi TANESCO, huwa hatuna bima ya afya baada ya kustaafu, kwahiyo tungeona hilo liangaliwe.

"Angalau kuwekwe utaratibu fulani hivi kama ilivyo serikalini, mfanyakazi akistaafu anaendelea kupatiwa matibabu kwa mpango maalum, ninafikiri hili linaweza kusaidia sana kuhakikisha kwamba sisi tuliochangia kuleta maendeleo ya nchi hii kwa miaka kadhaa iliyopita, kuwa na afya njema na tukaendelea kushiriki kuchangia maendeleo ya nchi yetu," alisema mmoja wa wastaafu hao.

Katibu wa umoja huo, James Chinula aliomba serikali kuendelea kuwatumia katika shughuli mbalimbali pale wanapowahitaji.

"Licha ya kustaafu, tunaweza kufanya kazi kwa sababu tuna taaluma na hazifi, kwahiyo tuko tayari kuendelea kuitumikia serikali yetu pale inapotuhitaji," alisema.

HADITHI

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-20

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

Wewe umeshawahi kuwa askari halafu ukafukuzwa nini?" "Kwa nini dokta?" "Mmmh! Yaani unaonekana uko makini sana, muangalifu sana, halafu una tekniki zile zile, tena siyo askari wa kawaida." "Hapana, kawaida tu." "Unajua nini, hata ulipokuja kwenye zahanati yangu, mbinu uliotumia hadi tukakupa kitanda ukakaa pale wiki mbili, sidhani kama kuna mtu anaweza kuwa na akili kama hiyo ya kuishi hospitalini ambapo hakuna askari anayeweza kumtafuta mhalifu. Halafu uliponifahamisha tu kuwa wewe ndiye yule unayetafutwa kwa kumuua mpenzi wako, ukahama pale, hukulala tena pale, hizo zote ni mbinu za kipelelezi tu." Dokta Shija akafunguka. Maneno hayo yalimfanya Kamal kuangua kicheko. Hakujibu kitu. "Tuyaache hayo. Kuna kitu ambacho nimekipata kwa ile kazi uliyonituma, tukae tu ndani ya gari itabidi tuzunguke tu, twende mpaka Buruguni, tukate mpaka Tabata, Ubungo, Magomeni, turudi Ilala Boma mpaka hapa hapa tena Kariakoo nikuteremshe, nadhani mazungumzo yatakuwa yamekamika, nitakuwa naendesha taratibu." Kamal alikuwa amekaa kimya na makini alimsikiliza Dokta Shija ni kitu gani ambacho ataka kumwambia ambacho kinaweza kumpa mwangaza wa nani yupo nyuma ya mauaji ya mpenzi wake, Mariamu hadi yeye kusingiziwa kuwa ndiye alimuua?

"Mimi nimeanza kuifanya kazi uliyonipa." Dokta akaanzisha mazungumzo. Moyo wa Kamal ukaanza kwenda kasi, kwani alijua sasa huenda kile alichokuwa akikitamani, kumpata muuaji wa Mariamu kinaweza kukamilila "Enhe dokta lete maneno." "Sikiliza kijana, hili suala lako ni kubwa na gumu sana kuliko unavyofikiria. Kufanya kazi mwenyewe tu haiwezekani. Huwezi kuwapata. Hata mimi mwenyewe siwezi kukusaidia mimi tu." Ni kama Kamal alikuwa amerudishwa nyuma. Mwanzoni kama alipewa matumaini, lakini sasa ni kama anakatishwa tamaa. Hakusema chochote, akabaki ameachama mdomo.

"Mimi nilivyoongea na madaktari wenzangu kuhusu aliyeratibu kubadilishwa kwa ripoti ya uchunguzi, ni kwamba nyuma ya pazia kuna mtu mkubwa tu, ambaye aliwaamrisha mabosi wa ngazi za juu ili kufanya hivyo. Na wote walihongwa. Madaktari waliofanya uchunguzi nao wakala chao, ikatoka ile ya kwanza kuwa alianguka mwenyewe kwenye mtaro kwa shinikizo la damu wakati akikimbia jogging. Inavyoonekana ni kwamba marehemu alivishwa nguo za mazoezi akiwa tayari ameshauawa na kwenda kutupwa Tabata.




"Mimi nilivyoongea na madaktari wenzangu kuhusu aliyeratibu kubadilishwa kwa ripoti ya uchunguzi, ni kwamba nyuma ya pazia kuna mtu mkubwa tu, ambaye aliwaamrisha mabosi wa ngazi za juu ili kufanya hivyo. Na wote walihongwa. Madaktari waliofanya uchunguzi nao wakala chao, ikatoka ile ya kwanza kuwa alianguka mwenyewe kwenye mtaro kwa...

Tumegundua hivyo baada ya uchunguzi wa pili uliowashirikisha madaktari ambao hawakuhongwa, nikiwemo mimi na hii ilitokana na kelele za ndugu wa marehemu na wananchi."

Kamal alimsikiliza kwa makini Dokta Shija aliyekuwa akiongeza huku akibadilisha gia, gari likiendelea kutafuna lami. Gari moja kati ya zile chache zilizobaki, ambazo dereva anaingiza gia si za kuingia zenyewe.

"Viashiria vilionyesha kuwa aliuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani, halafu wakenda mahali, wakaivua nguo ambazo marehemu alivaa, wakamvisha za mazoezi, lengo lilikuwa ni hilo hilo ionekane ameanguka mwenyewe akikimbia, na hata matokeo ya uchunguzi wa ripoti ya kwanza ulikuwa ni elekezi, yaani umetoka kwa wauaji wenyewe. Sasa ndugu yangu kama wauaji wamewapata mpaka mabosi wetu na kuwahonga, si watu wa kawaida, wala wa mchezo mchezo."

"Hata mimi nadhani hivyo Dokta." "Ukitaka kuamini hilo, sisi baada ya kutoa ripoti ya ukweli, ili kuendelea kuficha ushahidi wakatengeneza mazingira ambayo wewe ndiyo ukaonekana muuaji. Na hawa watu pia wamepenya pia Polisi, kuna baadhi wamekula mlungula ndiyo maana unatafutwa ndugu yangu." "Ni sahihi kabisa Dokta." "Sasa nikuulize kitu?" "Ndiyo." "Labda umeshawahi kutishiwa hivi, au mpenzi wako kutishiwa kabla ya kuuawa?" "Ndiyo, wote wawili tumetishiwa kwa nyakati tofauti na mimi ilikuwa bado kidogo nimuache kwa woga." Dokta akaangia kicheko halafu akamuuliza "Ulitumiwa meseji au kupigiwa simu?" "Mimi sikupigiwa simu, ni meseji tu, nina meseji mbili ambazo nimetishiwa." "Kwa namba tofauti?" "Ndiyo! Bahati nzuri au mbaya marehemu Mariamu naye ametishiwa mara mbili, na meseji ninazo pia!" "He! Kwani simu ya mpenzi wako unayo?" "Ninayo Dokta, kwa sababu alipotoka siku hiyo aliyouawa alikuwa ameisahau kwenye chaji. Na nilianza kuhisi kuna kitu baada ya kuona ikiita kwa muda mrefu bila kupokelewa, ikabidi haraka niende kwake, mlango ulikuwa umefungwa, lakini nina funguo za akiba, kuingia nikaikuta. Na tukio hili la kwenda kwake ghafla ndilo polisi wanalihusisha kuwa mimi nimemuua."

"Waliokutishia wewe au mpenzi wako walikuwa wanatishia nini hasa?" "Mimi wananiambia kuwa nimuache, siyo saizi yangu, siwezi kuwa na mwanamke mzuri kama yule wakati mimi ni fukara, na kama sitoweza kufanya hivyo wataniua." "Mpenzi wako je?" "Yeye naye alikuwa anaambiwa aniache, ananing'ang'ania kama luba mtu ambaye hana pesa, na wakamwambia kama akiendelea naye watamuua. Kuna meseji alikuwajibu kuwa hata mkimuua, hamuwezi kunipata kwa sababu na yeye atajiua. Nadhani hilo jibu liliwakasirisha hao watu wakaamua kumtoa yeye uhai."

"Sasa nikwambie kitu, hapa inaonekana pamoja na kwamba watu wengine wameshiriki hili, lakini mpenzi wake alikuwa anakiwa na mtu mmoja tu ambaye ndiye tunamsaka." "Nadhani Dokta."

"Na yeye ni mtu mwenye uwezo wa kipesa, tajiri au mwenye wadhifa hivi, aliyekuwa akitaka kutumia nguvu yake kukunyang'anya mpenzi na aliposhindwa akafanya hivyo na sasa anajaribu kuficha ushahidi kwa gharama zozote." "Sawa kabisa Dokta." "Sasa ulizifahamu namba hizo zote ni za nani?"

"Kusema kweli namba za meseji zangu mbili ni tofauti na za kwenye simu ya Mariamu pia ni mbili tofauti. Na kwa bahati mbaya nilijaribu kujifanya kama natuma pesa kwao, lakini mtandao ulijibu kuwa hazikuwa zimesajiliwa." "Da pole sana. Hawa watu walikuwa wamejipanga hasa." "Sasa kuna ndugu yangu mmoja, mdogo wangu, yeye ni askari polisi kitengo cha IT, suala lako limenigusa sana ilibidi nimuelezee hata kama wewe mwenyewe ulikuwa hupendi, lakini nimefanya hivyo wakati mwingine kwa ajili tu ya msaada. Ameniambia kama namba zipo basi unipe nimpelekee na jambo la kwanza atakalolifanya ni kujua zimesajiliwa wapi na waliozisajili ni akina nani."

"Ha! Dokta, utakuwa ni msaada mkubwa kwangu. Unajua mwanzoni sikukuamini kabisa nilipojitambulisha kwako, nikajua unaweza kuniuza kwa wanaonitafuta, lakini mpaka umefikia huko, ina maana kweli umemua kunisaidia." Kamal aliongea kwa furaha na bashasha, kwani alijua sasa hayupo peke yake. Kuna mtu amemua kumpigania na jambo hilo gumu linalomkabili.

**Itaendelea Jumamosi**

# KMC FC YAMNASA KIPA WA VIPERS, IKIWAZA 'TOP FOUR'

**Na Adam Fungamwango**

SIKU moja tu baada ya kumtambulisha kiungo mshambuliaji aliyekuwa akiichezea Kakamega Home Boys inayoshiriki Ligi Kuu Kenya, KMC FC imetangaza kumsajili kipa, Fabien Mutombora, raia wa Burundi, akitokea Vipers ya Uganda, imeelezwa.

Ofisa Habari wa KMC, Khalid Chukuchuku, alisema jijini Dar es Salaam jana, usajili huo umefanyika katika malengo ya kuimarisha kikosi chao kutokana na ushindani uliopo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Chukuchuku alisema wanataka kuona timu yao inafanya vizuri katika mashindano yote watakayoshirili kwenye msimu ujao.

Alisema kipa huyo amesajiliwa kwa matakwa na Kocha Mkuu, Abdihamid Moallin, ambaye amedhamiria kukiongezea nguvu kikosi chake.

"Tumemnasa kipa mzuri na bora kabisa, ni matakwa ya kocha na benchi la ufundi, mpaka sasa tumeshasajili wachezaji watatu na bado tunaendelea kuboresha kikosi chetu kwa sababu msimu ujao tunataka kumaliza ndani ya nafasi nne bora za juu," alisema Chukuchuku.

Mutombora mwenye umri wa miaka 27, alizaliwa Bujumbura na kabla kujiunga na Vipers mwaka 2018, aliichezea klabu ya LLL Academic ya Burundi.

Kipa huyo anakuwa mchezaji wa tatu kutambulishwa na klabu hiyo, ambapo ilianza kwa kumsajili kinda wa zamani wa Mtibwa Sugar, ambaye kwa sasa anachezea Timu ya Taifa ya vijana chini ya miaka 20, Nickson Mosha, anayecheza beki wa kati, kabla ya kumtangaza kiungo mshambuliaji, Oscar Paul.

Wakati huo huo KMC imemwongezea mkataba kocha wake Moallin, ili aendelee kukinoa kikosi hicho kwa mara nyingine tena msimu ujao.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Soka la Ufukweni wakifanya mazoezi kwenye ufukwe wa Coco kwa ajili ya kujiandaa na mechi za kufuzu kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (BSAFCON), zitakazofanyika baadaye mwaka huu. **PICHA: TFF**

# KLABU BINGWA NETIBOLI AGOSTI

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Klabu Bingwa Taifa ya netiboli yanatarajiwa kufanyika kuanzia Agosti Mosi hadi 12, mwaka huu jijini, Arusha.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), Devota Marwa, alisema lengo la mashindano hayo yatashirikisha timu zote za Daraja la Kwanza.

Marwa alisema michuano hiyo itatoa timu sita zitakazokwenda Zanzibar kushiriki mashindano ya Afrika Mashariki yatakayofanyika hapo mwakani.

Alisema mwisho wa timu kuthibitisha ushiriki wao ni Julai 28, mwaka huu na kufanya hivyo itasaidia katika kukamilisha maandalizi.

"Maandalizi kwa ajili ya mashindano haya yameshaanza na timu zitakazoshiriki zinatakiwa kuthibitisha kama taratibu zinavyoelekeza, yanafanyika mapema ili kupata wawakilishi muda wa kujiandaa," alisema Marwa.

Aliongeza mashindano hayo pia yatasaidia kupata Timu ya Taifa na wanatarajia kushuhudia ushindani kutoka kwa nyota vijana.

"Ninaomba wadau mbalimbali wajitokeze kwa wingi wakati wa mashindano ili kushuhudia vipaji vitakavyoonyeshwa na wachezaji wetu, " Marwa aliongeza.

## Beki mpya Mganda atua Coastal Union

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Coastal Union imetangaza kumsajili beki wa kati, Anguti Luis, kutoka KCCA ya Uganda.

Ofisa Habari wa Coastal Union, Abbas El Sabri, ameliambia gazeti hili beki huyo mwenye uwezo wa kucheza namba nne na tano, amesajiliwa na klabu hiyo kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye safu ya ulinzi huku wakielekea katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Kama mnavyojua, hatujawahi kufanya makosa katika kuchagua mabeki wa kati, sasa tumemleta mjukuu wa Yoweri Museveni (Rais wa Uganda), ni kijana mdogo mwenye miaka 18 tu, lakini atapewa jukumu la kuilinda ngome ya Coastal Union," alisema Sabri.

Mtihani kwa kwanza wa beki huyo utakuwa katika michuano ya Kombe la Kagame inayotarajiwa kufanyika kuanzia Jumanne hapa jijini, Dar es Salaam.

Beki huyo anatajwa kuziba nafasi ya mlinzi mwingine aliyeondoka, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Felly Mulumba, lakini pia Lameck Lawi, ambaye usajili wake wa kuelekea Simba bado umegubikwa na sintofahamu.

## Kocha wa Namungo kujulikana rasmi leo

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Namungo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kumtambulisha kocha wake mpya ambaye atawasili Ruangwa mkoani, Lindi leo akitokea kwao Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Katibu Mkuu wa Namungo FC, Abdallah Mkadeba, alisema mara baada ya kocha huyo kuwasili, anatarajiwa kuanza kibarua chake leo.

"Muda wowote kuanzia sasa kocha wetu atawasili kwa ajili ya kuanza rasmi mazoezi hapo kesho ( leo) ili kujiandaa na msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, tunaanza maandalizi mapema kwa sababu hatutaki kuwa na msimu mbaya," alisema Mkadeba.

Alisema malengo ya Namungo kuelekea msimu ujao ni kufanya vyema katika kila mechi huku wakidhamiria kumaliza msimu wakiwa kwenye nafasi za juu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tutahakikisha tunafanya vizuri na tunakata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa, hatutabweteka, tutapambana katika kila mechi," alisema katibu huyo bila kutaja jina la kocha mpya waliyemnasa.

## ZISIKUPITE

### EDERSON ATAKIWA SAUDIA

KLABU ya Manchester City inajiandaa kupokea ombi kutoka Saudi Arabia la kumnunua mlinda mlango, Ederson na wanataka zaidi ya pauni milioni 30 kumuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, ambaye anahusishwa na Al-Nassr. ***(Sportsport)***

### GREENWOOD KUTUA MARSEILLE

MARSEILLE ina uhakika wa kuwashinda Lazio katika vita ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood, baada ya klabu hiyo ya Serie A kutoa pauni milioni 17 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Mail)***

### WEST HAM, FAMENGO KUTETA

FAMENGO imefanya mawasiliano na West Ham kuhusu usajili wa mchezaji wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 26, Lucas Paqueta, huku klabu hizo mbili ziko katika hatua za awali za mazungumzo. ***(Globo)***

### WILLIAMS AKARIBIA BARCA

BARCELONA inaongoza katika mbio za kumsajili winga wa Athletic Bilbao na Timu ya Taifa ya Hispania, Nico Williams, huku Arsenal na Chelsea wakikabiliwa na hatari ya kumkosa mchezaji huyo. (Football Insider)

### CUCURELLA AMTAKA WILLIAMS

MLINZI wa Chelsea, Marc Cucurella, ambaye ana umri wa miaka 25, amesema anajaribu kumshawishi mchezaji mwenzake wa Hispania, Nico Williams, ili ajiunge na The Blues, wawili hao wapo kwenye kikosi cha nchi yao kinachoshiriki michuano ya Euro 2024. ***(Sport)***

### YORO AGOMBEWA ULAYA

MLINZI wa Lille, Leny Yoro, anataka kuhamia Real Madrid na Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 18 anasubiri kabu kuafikiana, wakati Liverpool na Paris St-Germain ziko tayari kumnyakua iwapo dili hilo litasambaratika. ***(Fabrizio Romano)***

### MATTY AOTA MBAWA

MLINZI wa kulia wa Aston Villa, Matty Cash, huenda asijiunge na AC Milan licha ya ripoti zinazomhusisha mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland mwenye umri wa miaka 26 na klabu hiyo inayoshiriki Serie A. ***(Birmingham Live)***

### CANCELO AIVUTIA BARCA

BARCELONA imeonyesha nia ya kumsajili, Joao Cancelo, wa Manchester City baada ya beki huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 30 kucheza kwa mkopo katika klabu hiyo ya Hispania msimu uliopita. ***(SportsMole)***

### JUVE YAMFUATA KOOPMEINERS

JUVENTUS inataka kuimarisha safu yao ya kati kwa kumsajili mchezaji wa kimataifa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 26, Teun Koopmeiners. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### LUSALE KUTUA UNITED

KLABU ya Manchester United inakaribia kumsajili kinda mwenye umri wa miaka 16 kutoka Slovakia, Samuel Lusale, kutoka Crystal Palace. ***(Moror)***

### DOMINIC AIKWAMISHA EVERTON

MCHAKATO wa Newcastle United kumtaka mshambuliaji wa Everton, Dominic Calvert-Lewin, mwenye umri wa miaka 27, umegonga mwamba baada ya Magpies kushindwa kumuuza nyota wao, Callum Wilson. ***(Telegraph)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MARTINEZ AWA SHUJAA WA ARGENTINA COPA

●●● Kipa huyo aokoa penalti mbili na kuipeleka timu yake nusu...

**HOUSTON,** MAREKANI

ARGENTINA iliifunga Ecuador penalti 4-2 na kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Copa América baada ya kipa, Emi Martinez, kuokoa mara mbili kufuatia sare ya 1-1 katika muda wa kawaida katika mechi iliyochezwa juzi.

Mechi hiyo ilienda kwa mikwaju ya penalti baada ya bao la kwanza la Lisandro Martínez wa Argentina kufutwa na Kevin Rodríguez katika dakika za majeruhi. Hakuna muda wa ziada katika michezo ya mtoano ya Copa América, isipokuwa mechi ya fainali.

Katika mikwaju hiyo, Lionel Messi alikosa ya kwanza, lakini Martinez aliokoa penalti za Ángel Mena na Alan Minda na sasa mabingwa hao watetezi wametinga nusu fainali watakayocheza dhidi ya Venezuela au Canada.

"Katika mikwaju ya penalti, timu ina imani na mlinda mlango wake na hilo ni la msingi," alisema Kocha wa Argentina, Lionel Scaloni.

"Hata baada ya kukosa kwa Leo na kwa kila njia kwa timu, ni muhimu sana kipa wetu atuokoe.

„Nadhani haifurahishi unaposhinda kwa njia hii. Bila shaka, tuna furaha, lakini sikufurahia ushindi huu."

Messi alianza mchezo huo licha ya kuwa majeruhi baada ya kukosa mechi yao ya mwisho ya hatua ya makundi dhidi ya Peru kutokana na tatizo la misuli ya paja, na nahodha huyo wa Argentina alivunja rekodi ya kucheza kwa dakika nyingi katika historia ya michuano hiyo.

"Messi alimaliza mchezo vizuri, mara ya mwisho tulipomuuliza zikiwa zimesalia dakika tano au sita kabla ya mchezo kumalizika alisema anajisikia vizuri," alisema Scaloni.

Argentina walitawala mpira mapema, lakini ni Ecuador ambao walitengeneza nafasi ya kwanza wakati Jeremy Sarmiento alipopata nafasi ya kupiga shuti kutoka pembeni na kumlazimisha Martinez kuokoa. Lakini mashabiki wa Argentina walipopata sauti zao, timu yao ilichukua uongozi katika dakika ya 35 baada ya mpira wa kichwa uliopigwa na Alexis Mac Allister kumkuta Martinez kwenye lango la mbali na beki huyo akafunga bao lake la kwanza la kimataifa.

Ecuador waliongeza shinikizo katika kipindi cha pili na matokeo yakazaa kona kwenye dakika ya lala salama wakati krosi ilipoelekezwa kwenye mkono wa Rodrigo De Paul na mwamuzi akaelekeza moja kwa moja ni penalti.

Nahodha, Enner Valencia alipiga hatua na kumpeleka Martinez kwa njia mbaya, lakini mfungaji bora wa Ecuador aliona jitihada zake zikitoka nje ya lango kabla ya beki wa Argentina Cristian Romero kuzuia shuti lililotoka kwa mpira uliorudiwa.

# UNITED YAMPA TEN HAG MKATABA MIAKA MIWILI

**MANCHESTER,** ENGLAND

ERIK ten Hag amesaini mkataba mpya wa kuendelea kuinoa Manchester United hadi Juni mwaka, 2026.


Ten Hag na United hawakuwa na msimu wenye kuridhisha ambapo timu ilimaliza Ligi Kuu England ikiwa nafasi ya nane pamoja na kuondolewa katika hatua ya makundi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ikishika mkia katika Kundi A.

Hii ilipelekea hatima ya Ten Hag kutojulikana huku vyombo vingi vikiripoti huenda angetimuliwa klabuni hapo.

Hata hivyo, Ten Hag aliiwezesha klabu hiyo kutwaa taji la FA na kufuta machungu ya msimu huo mgumu.

Baada ya kusaini mkataba huo mpya, Ten Hag alisema; "Nimefurahi kufikia makubaliano na klabu kuendelea kufanya kazi pamoja. Nikiangalia miaka miwili nyuma, tunaweza kuvuta picha na kujivunia makombe mawili na mifano mingi ya maendeleo kutoka hali niliyoikuta nayo timu na sasa.

"Lakini,tunatakiwa kuweka wazi kuna kazi kubwa zaidi ya kufanya kufikia ukubwa unaotakiwa wa Manchester United, yaani kuwania ubingwa wa Ligi Kuu na mataji ya Ulaya."



## Raya mali rasmi ya Arsenal


**LONDON,** ENGLAND

KLABU ya Arsenal hatimaye imekamilisha usajili kwa mkataba wa kudumu kwa golikipa wao namba moja, David Raya.

Washika bunduki hao wa jiji la London wamekamilisha usajili huo baada ya majadiliano ya muda mrefu na klabu yake mama ya Brentford kwa kumpa mkataba wa muda mrefu.

Arsenal wamelipa pauni milioni 27 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania, wakijazia ya ada ya pauni milioni tatu waliyowalipa Brentford walipomchukua Raya kwa mkopo msimu uliopita.

Raya alikuwa kiungo muhimu katika mafanikio ya klabu ya Arsenal kumaliza nafasi ya pili katika Ligi Kuu England na robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Alicheza mechi 32 na kutoruhusu bao katika michezo mechi 16, akishinda mechi 23 na kupoteza michezo mitano pekee.







## Cucurella amtaka Williams Chelsea

**BERLIN,** UJERUMANI

BEKI wa Chelsea, Marc Cucurella amekiri kuwa amekuwa akijaribu kumshawishi winga wa Athletic Club, Nico Williams kuhamia Stamford Bridge msimu huu wa joto.

Wawili hao wote wapo na kikosi cha Hispania kwenye michuano ya Euro 2024, ambapo Williams anatarajiwa kupokea nia kubwa ya kuhama kutoka kwa klabu kote Ulaya.

Barcelona wanajulikana wanamtaka zaidi Williams, lakini Cucurella akikiri winga huyo atakuwa usajili mzuri Camp Nou, huku akimsihi kuhamia Chelsea badala yake.

"Ni mchezaji mzuri, anadhihirisha uwezo wake wote, ni jambo la kujivunia yuko kwenye timu yetu, ni mwenzetu na kwa wachezaji kama yeye kila kitu ni rahisi," alisema Cucurella akiiambia SPORT.

"Atakuwa usajili mzuri kwa Barcelona, lakini ninamsukuma kusaini Chelsea. Mwishoni yote inategemea yeye. Yeye ni mdogo sana, na uzoefu mkubwa, na nadhani atakuwa mchezaji mzuri."

AS hivi majuzi iliripoti Chelsea iko tayari kuanzisha kifungu cha kutolewa kwa Williams cha euro milioni 58, ingawa inaelewa The Blues ni miongoni mwa pande zinazohusika na madai ya mshahara mkubwa wa winga huyo.

"Tulizungumza na nikamwambia ikiwa anahitaji chochote, anifahamishe," alisema Cucurella.

„Nina furaha kwa sababu ni mchezaji mkubwa, mdogo sana, mwenye mustakabali mzuri sana na tutamtunza ili aweze kucheza soka lake bora."

# VALENTINO ASAJILIWA SIMBA, WACHEZAJI WAPIMWA AFYA

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI wachezaji wa Simba wakifanyiwa vipimo vya afya kwa ajili ya kuanza rasmi maandalizi ya msimu mpya wa mashindano, Wekundu wa Msimbazi wamefanikiwa kumsajili aliyekuwa mshambuliaji wa Geita Gold FC, Valentino Mashaka.

Taarifa zilizotolewa na uongozi wa Simba zinasema Valentino amesaini mkataba wa miaka miwili.

"Rasmi Valentino Mashaka ni mnyama," ilisema kwa kifupi taarifa ya Simba.

Simba imeendelea kuimarisha kikosi chake baada ya jana kutangaza wamemsajili mshambuliaji mwingine Mtanzania, Abdulrazak Hamza, ambaye alikuwa akicheza soka la kulipwa Afrika Kusini.

Wakati huo huo, wachezaji wa Simba ambao wako nchini jana walifanyiwa vipimo vya afya maalumu kabla ya kuanza mazoezi kuelekea msimu mpya.

Nyota waliofanyiwa vipimo ni wapya pamoja na wale wa zamani ambao wameongezewa mikataba ya kuendelea kuitumikia klabu hiyo ya Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema utaratibu huo hufanyika kila mwaka kabla wachezaji hawajaingia kambini.

Ahmed alisema baada ya kumaliza zoezi hilo, wachezaji watajiandaa na safari ya kuelekea Misri ambapo wanakwenda kuweka kambi ili kujiandaa na msimu mpya.

Simba iliyomaliza msimu uliopita katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, inatarajia kumtangaza rasmi Fadluraghman Davids, kama kocha mpya ambaye anarithi mikoba iliyoachwa na Abdelhakh Benchikha.



Wachezaji wa Azam FC wakiwa katika mazoezi ya kwanza kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa mashindano ya mwaka 2024/2025. **PICHA: MTANDAO**

# Coastal, Dekedaha kufungua Kagame

**Na Somoe Ng'itu**

COASTAL Union itaanza kampeni ya kuwania ubingwa wa Kombe la Kagame kwa kuivaa Dekadaha FC kutoka Somalia katika mechi ya Kundi A itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa KMC uliokо Mwenge, Dar es Salaam.

Mechi nyingine itakayochezwa kwenye uwanja huo siku ya ufunguzi itakuwa ni kati ya Al Wahdi kutoka Sudan dhidi ya JKU SC ya Zanzibar. Ratiba ya michuano hiyo inaonyesha usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, Waganda SC Villa watakutana na Al Merreikh Bentiu ya Sudan huku APR ya Rwanda watavaana na Singida Black Stars ya mkoani Singida.

Julai 10, mwaka huu, Al Hilal ya Sudan Kusini itacheza dhidi ya Djibout Telecom huku Gor Mahia FC ya Kenya itawaalika mabingwa wa Ligi Kuu Zambia, Red Arrows, mechi zote zikifanyika kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Meneja Mashindano wa Baraza la Soka la Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Baraka Kizuguto, aliliambia gazeti hili timu nne zitakazofanya vizuri zitasonga mbele hatua ya nusu fainali ambayo itachezwa Julai 19, mwaka huu.

Kizuguto alisema fainali ya mashindano hayo itachezwa Julai 21, mwaka huu na itatanguliwa na mechi ya kusaka mshindi wa tatu.

## Baleke asajiliwa

INATOKA UK. 24

Kasongo, amesema Ligi Kuu itaanza Agosti katikati, ikiwa ni wiki moja baada ya kumalizika kwa Ngao ya Jamii itakayochezwa Agosti 11, mwaka huu.

"Tupo kwenye maandalizi ya ratiba, ligi yetu itaanza katikati ya mwezi wa nane, nadhani baada ya ile wiki ya mechi za Ngao ya Jamii, basi wiki inayofuata ligi inakwenda kuanza. Ukiangalia ratiba, tarehe 8 ni mechi ya kwanza, tisa ya pili, tarehe 10 ni mapumziko, Agosti 11 ni fainali, wiki moja tu baadaye ligi inaanza rasmi," alisema Kasongo.

Alikumbusha kwa mara nyingine tena msimu ujao kwa mara ya kwanza Ligi Kuu itatumia teknolojia ya video ya kumsaidia mwamuzi VAR, ingawa si kwa mechi zote.

"Kingine pamoja na tutaitumia VAR, lakini bado haiwezi kumaliza tatizo, kwa sababu kwa mujibu wa FIFA yenyewe inasimamia mambo matatu, utata wa kadi nyekundu, kuotea na penalti, haihusiki na bao, mambo mengine wanawaachia waamuzi wenyewe, mfano mechi ya Yanga na Mamelodi Sundowns, watu wa VAR waliwaachia wenyewe kwa sababu siyo katika vitu ambavyo inapaswa kuviamua.

Kwa maana hivyo pamoja na kuwapo kwa VAR, waamuzi bado wanatakuwa wawe makini na wachezeshe kwa uangalifu," Kasongo aliongeza.

## Majaliwa: Tutaibeba Stars AFCON 2027

INATOKA UK. 24

na kinga, usafiri, ulinzi na usalama, sheria, masoko, matangazo, uendeshaji matukio, usimamizi wa timu, mashabiki na watazamaji.

Naye Tenga alisema kamati hiyo itafanya kile kinachostahili ili nchi iweze kufanikiwa na kufanya vizuri katika michuano ya AFCON 2027.

"Tunaipongeza Serikali kwa kutuletea watu makini kwa ajili ya kufanikisha AFCON 2027."

Kwa upande wake, Rais wa TFF, Wallace Karia, ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuwa mdau mkuu ikiwamo kuweka mazingira rafiki ya kuendesha shughuli za michezo nchini.

"Kwetu sisi kipaumbele ni suala la AFCON."

Karia pia ameishukuru Serikali kwa kuwa na wazo la muda mrefu la kuandaa michuano ya AFCON.

"Hatimaye tumefanikiwa, tunashukuru, leo tupo hapa tunazindua kamati na itakabidhiwa majukumu."

Msitha ambaye ni Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), alisema wazo la Tanzania kuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON lilitolewa na TFF, na mchakato huo ulianza mara moja na kufanikiwa kupata fursa hiyo.

„Tanzania Kenya na Uganda tuliamua kuungana pamoja kuwa wenyeji, nchi nyingi ziliomba lakini Tanzania ilishinda kutokana utayari wa kisiasa tulionao pamoja na ushirikiano mzuri wa viongozi," alisema Msitha.

Michezo
Nipashe Jumamosi Julai 6, 2024

**Martinez awa shujaa wa Argentina Copa**
UKURASA 21



●●● Guede atemwa rasmi, fainali ya Ngao ya Jamii kuchezwa Agosti 11...

# Baleke asajiliwa Yanga

**Somoe Ng'itu na Adam Fungamwango**

WAKATI wachezaji wa Yanga wakitarajiwa kuanza maandalizi ya msimu ujao Jumatatu, klabu hiyo imekamilisha usajili wa mshambuliaji wa zamani wa Simba, Jean Othos Baleke.

Simba iliachana na mshambuliaji huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), katika dirisha dogo la usajili, akiwa ndiye nyota mwenye mabao mengi ndani ya kikosi cha Wekundu wa Msimbazi.

Mshambuliaji huyo alikuwa akionekana zaidi katika mechi za Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), wakati mabingwa wa ligi hiyo, Simba Queens walipokuwa wakicheza.

"Baleke amesajiliwa Yanga na anachukua nafasi ya Joseph Guede, ambaye alisajiliwa kwa miezi sita tu, Beleke amepata nafasi ya kusajiliwa kwa sababu anaijua Tanzania, ameshazoea mazingira na ligi yenyewe pamoja na viwanja, viongozi wanaamini kuwa yeye ni mtu sahihi," kilisema chanzo chetu.

Taarifa zaidi zinasema Baleke, ambaye alitua Simba kwa mkopo mwaka jana akitokea TP Mazembe ya DRC, amesaini mkataba wa miaka miwili.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema wana orodha ndefu ya wachezaji wapya ambao wataitumikia timu hiyo katika msimu mpya wa mashindano wa mwaka 2024/2025.

"Bado kuna orodha ndefu kidogo ya wachezaji wapya ambao wataingia kwenye kikosi cha Yanga kuelekea msimu ujao, hapa ni wale wa ndani na wa nje, tayari tumeshawasajili, tunaandaa utaratibu na mpangilio mzuri wa kuwatambulisha, tuangalia tuanzie wapi na tumalize vipi, Chama amekuwa wa kwanza kumtambulisha wengine watangazwa hivi karibuni.

Kamwe alisema Kocha Mkuu wa timu yao, Miguel Gamondi, amehitaji kuona nyota wote wanaripoti kambini keshokutwa kabla ya utaratibu mwingine kuelendelea.

"Kuhusu maandalizi ya msimu na kambi, wachezaji wetu wataanza kuingia Jumatatu, ,pre season' tutaweka wapi? Pale pale Kigamboni au tutasafiri? Tutakuja kuwajuza," Kamwe alisema.

Aliongeza Yanga imemwongeza mkataba kipa wake, Aboutwalib Mshery, ambao utamalizika ifikapo mwaka 2027 sawa na beki, Nickson Kibabage.

Katika hatua nyingine, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), Almasi

INAENDELEA UK. 23




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (katikati), akimkabidhi mwongozo, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Ndani ya Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON2027), Leodegar Tenga, katika hafla iliyofanyika jijini, Dar es Salaam jana. Kulia ni Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia. **PICHA: TFF**

# Majaliwa: Tutaibeba Stars AFCON 2027

**Na Shufaa Lyimo**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Serikali inaahidi itashirikiana na Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi ya Kombe la Mataifa Afrika (AFCON 2027), ili kuhakikisha Tanzania (Taifa Stars), inafikia malengo yake ya kufanya vizuri katika michuano hiyo.

Wajumbe walioko katika kamati hiyo ni pamoja na Leodegar Tenga atakayekuwa Mwenyekiti, Ayoub Mohammed Mahmoud (Makamu Mwenyekiti), Neema Msitha (Katibu Mkuu) na Said Kassim (Katibu Msaidizi) na mjumbe ni Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania TFF, Wallace Karia.

Majaliwa alisema hayo jana katika hafla maalum na kuongeza Serikali ina imani kubwa na kamati hiyo itapata mafanikio.

"Tuambieni tufanye nini ili tuwe mabingwa, kusanyiko hili liibue nini tufanye sasa na tuanze leo (jana), kufanya maandalizi. Tumeunda kamati yenye weledi na wataalamu kwenye sekta ya michezo, tunategemea itupeleke kwenye mafanikio makubwa. Uwepo wenu ni imani ya Serikali mnaweza kusimamia suala hili."

Aliongeza serikali imeendelea kufanya maandalizi ikiwamo maboresho ya miundombinu ya viwanja, barabara, reli, anga na usafiri wa maji.

"Serikali tumejiweka vizuri kuwa mwenyeji wa mashindano haya, sifa, uwezo na dhamira ya kufanikisha mashindano haya tunayo," Majaliwa alisisitiza.

Alisema mashindano hayo yataongeza idadi ya wageni na watalii hapa nchini, ambao watakuja kwa ajili ya kutazama mechi na matukio yanayohusiana na AFCON 2027.

"Hii itasaidia kuongeza mapato ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla."

Naye Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, alisema uzalendo na utashi wa kisiasa wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, umeifanya sekta ya michezo kusonga mbele na hatimaye kuiheshimisha sekta ya michezo nchini.

Ndumbaro alisema kamati hiyo itakuwa na kamati ndogo 13 za wataalamu na watu waliobobea katika maeneo mbalimbali. "Kamati zitakuwa za miundombinu, mawasiliano, fedha, tiba

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >